

Notisi ya Ulinzi wa Kiutaratibu: Haki za Wazazi wa Wanafunzi walio na Ulemavu



Tarehe ya Kuanza: Oktoba 19, 2022



Nyenzo

Msimamizi wa Elimu Maalum katika Wilaya ya Shule Yako

Yuko na habari kuhusu haki zako na huduma za elimu maalum katika jumuiya yako. Wasiliana na ofisi ya msimamizi wako ili upate jina na nambari ya simu ya mtu huyu.

Jimbo la Vermont: Wakala wa Elimu

Nyaraka ya [Haki za Wazazi wa Wanafunzi walio na Ulemavu](#) inatoa taarifa kuhusu upatanishi, mchakato faafu au malalamishi ya kiutawala, na mambo mengine yanayohusu haki za wazazi wa wanafunzi walio na ulemavu. Isitoshe, taarifa za mawasiliano zinaweza kupatikana katika nyaraka hii ikiwa utakuwa na maswali au shauku zozote.

Fomu

- [Fomu ya Upatanishi](#)
- Malalamishi ya mchakato faafu: [kwa wazazi](#)
- Malalamishi ya mchakato faafu: [kwa wilaya za shule](#)
- [Fomu ya malalamishi ya kiutawala](#)

Anwani ya barua pepe ya kuwasilisha fomu kwa njia ya kielektroniki:
AOE.MediationDPinfo@vermont.gov

Anwani ya posta ya kuwasilisha fomu kwa njia ya posta:

Shirika la Elimu

Huduma za Upatanishi wa Elimu Maalum

1 National Life Drive, Davis 5

Montpelier, VT 05620-2501

Nyenzo nyingine za kikanda

[Mtandao wa Familia wa Vermont](#)

600 Blair Park, Rd Ste. 240

Williston, Vermont 05495

Simu: (802) 876-5315

[Mradi wa Vermont wa Sheria za Ulemavu](#)

264 North Winooski Avenue

Burlington, VT 05401

Simu: (800) 889-2047

Yaliyomo

Nyenzo.....	2
Msimamizi wa Elimu Maalum katika Wilaya ya Shule Yako	2
Jimbo la Vermont: Wakala wa Elimu	2
Fomu	2
Nyenzo nyingine za kikanda.....	2
Notisi ya Ulinzi wa Kiutaratibu: Haki za Wazazi wa Wanafunzi walio na Ulemavu.....	8
Mchango wa Mzazi katika Kanuni za Elimu Maalum za Vermont.....	8
Mchango wa Mzazi katika maudhui kwenye IEP	9
Taarifa ya Jumla	10
Notisi ya Awali katika Maandishi	10
Notisi.....	10
Yaliyomo kwenye notisi.....	10
Notisi katika lugha inayoeleweka	11
Lugha ya Asili.....	11
Barua Pepe	11
Kibali cha Mzazi - Ufasili	11
Kibali cha Mzazi.....	12
Kibali kwa tathmini ya awali	12
Kanuni maalum kwa tathmini ya awali ya Watoto walio chini ya ulinzi wa Serikali.....	12
Kibali cha mzazi kwa huduma.....	13
Kubatilisha kibali cha mzazi kwa huduma.....	13
Kibali cha mzazi kwa tathmini mpya	14
Rekodi za juhudi faafu za kupata kibali cha mzazi	14
Mahitaji mengine ya kibali	14
Tathmini Huru za Kielimu	15
Jumla	15
Ufasili.....	15
Haki ya mzazi ya tathmini kwa gharama ya umma.....	15
Tathmini zinazoanzishwa na Mzazi.....	16
Maombi ya tathmini ya Maafisa waamuzi.....	16

Vigezo vya wilaya ya shule/muungano wa usimamizi.....	16
Usiri wa Taarifa.....	16
Ufasili.....	16
Inayomtambulisha Mtu Binafsi.....	17
Notisi kwa Wazazi.....	17
Haki za ufikiaji.....	17
Rekodi ya Ufikiaji.....	18
Rekodi kuhusu Zaidi ya Mtoto Mmoja.....	18
Orodha ya Aina na Maeneo ya Taarifa.....	18
Ada.....	18
Marekebisho ya Rekodi kutokana na Ombi la Mzazi.....	19
Fursa ya Kikao cha Kusikilizwa.....	19
Utaribu wa Kikao cha kusikilizwa.....	19
Matokeo ya Kikao.....	19
Kibali cha Ufichuzi wa Taarifa Inayomtambulisha Mtu Binafsi.....	20
Ulinzi.....	20
Uharibifu wa Taarifa.....	20
Taratibu za Malalamishi za Vermont.....	21
Tofauti kati ya Kikao cha Malalamishi kuhusu Mchakato Faafu na Taratibu za Malalamishi ya Kiutawala.....	21
Taratibu za Malalamishi ya Kiutawala.....	21
Jumla.....	21
Kuongeza Wakati.....	22
Malalamishi ya kiutawala na vikao vya mchakato faafu.....	22
Kuwasilisha Malalamishi ya Kiutawala.....	22
Jumla.....	23
Malalamishi ya Sehemu C.....	23
Taratibu za Malalamishi ya Mchakato Faafu.....	23
Kuwasilisha Malalamishi ya Mchakato Faafu.....	23
Jumla.....	23
Taarifa kwa wazazi.....	24
Malalamishi ya Mchakato faafu.....	24

Jumla	24
Maudhui ya Malalamishi	24
Notisi inahitajika kabla ya kikao cha malalamishi ya mchakato faafu	25
Utoshlevu wa Malalamishi	25
Marekebicho ya Malalamishi	25
Majibu ya wilaya ya shule au muungano wa usimamizi kwa malalamishi ya mchakato faafu	25
Majibu ya wahusika wengine kwa malalamishi ya mchakato faafu	26
Mifano ya Fomu	26
Upatanishi	26
Jumla	26
Mahitaji	26
Mpatanishi kutokuwa na upendeleo	27
Nafasi ya Mtoto wakati Malalamishi ya Mchakato faafu Yakisubiri Kusikizwa	28
Mchakato wa Kusuluhisha	28
Mkutano wa Kusuluhisha	28
Kipindi cha Upatanishi	29
Marekebicho ya kipindi cha kusuluhisha cha siku 30 za kalenda	30
Mkataba wa maafikiano katika maandishi	30
Kipindi cha kukagua Mkataba	30
Vikao vya Malalamishi ya Mchakato Faafu	30
Kikao cha Mchakato Faafu Kisichokuwa na Upendeleo	30
Afisa wa Mwamuzi wa Kikao Kisichokuwa na Upendeleo	30
Mada ya kikao cha mchakato faafu	31
Ratiba ya kuomba kikao	31
Kutozingatia ratiba	31
Haki za kikao	31
Jumla	31
Ufichuzi wa ziada wa taarifa	32
Haki za mzazi katika vikao	32
Maamuzi ya Kikao	32
Maamuzi ya Afisa mwamuzi	32

Kifungu cha Masharti ya jumla.....	33
Ombi tofauti la kikao cha mchakato faafu.....	33
Matokeo na uamuzi kwa jopo la ushauri na umma kwa jumla	33
Rufaa	33
Makataa ya Uamuzi; Rufaa; Ukaguzi Usio na Upendeleo.....	33
Makataa ya Uamuzi wa Kikao	33
Ratiba na Urahisi wa Vikao na Ukaguzi.....	33
Kesi za Madai, Ikiwemo Kipindi cha Muda ambacho Kesi hizo Zinapaswa Kuwasilishwa....	34
Jumla	34
Kikomo cha Muda.....	34
Taratibu za ziada	34
Mamlaka ya mahakama za wilaya	34
Kanuni ya Masharti ya jumla	34
Ada za wakili	35
Jumla	35
Fidia za ada	35
Taratibu Wakati wa Kuadibu Watoto Walio na Ulemavu.....	36
Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule	36
Uamuzi kwa kila kesi	36
Jumla	37
Mamlaka ya Ziada	37
Huduma	37
Uamuzi wa Udhihirisho.....	38
Uamuzi kwamba mwenendo ulikuwa udhihirisho wa ulemavu wa mtoto	38
Hali za Kipekee	39
Ufasili.....	39
Taarifa	39
Kubadilisha Nafasi Kwa Sababu ya Uondoaji wa Kinidhamu	40
Uamuzi wa Mazingira.....	40
Rufaa	40
Jumla	40

Mamlaka ya afisa mwamuzi.....	40
Nafasi Wakati wa Rufaa.....	41
Ulinzi Kwa Watoto Ambao Bado Hawastahiki Elimu Maalum na Huduma Zinazohusiana..	41
Jumla	42
Msingi wa ufahamu kwa masuala ya kinidhamu	42
Hali za pekee.....	42
Masharti ambayo yanatumika ikiwa hakuna msingi wa ufahamu	42
Rufaa Kwa na Hatua Za Maafisa wa Sheria na Mamlaka za Mahakama	43
Utumaji wa rekodi	43
Mahitaji ya Uamuzi wa Kibinafsi wa Wazazi wa Watoto Kuwasajili Katika Shule ya kibinafsi kwa Gharama ya Umma	43
Jumla	43
Urejeshaji kwa usajili katika shule ya kibinafsi	44
Ukomo wa Urejeshaji	44

Notisi ya Ulinzi wa Kiutaratibu: Haki za Wazazi wa Wanafunzi walio na Ulemavu

Sheria ya Elimu ya Watu walio na Ulemavu (IDEA), sheria ya Shirikisho kuhusiana na elimu ya wanafunzi walio na ulemavu, inazihitaji shule kuwapa wazazi wa mtoto aliye na ulemavu notisi iliyo na maelezo kamili ya ulinzi wa kiutaratibu uliopo kwa mujibu wa IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Wakala wa Elimu wa Vermont (Marejeleo yote kwa kanuni hizi yanaweza kupatikana kupitia [Mwongozo wa Kanuni na Desturi za Bodi ya Elimu ya Jimbo la Vermont](#); marejeleo kwa Kanuni ya 34 ya Kanuni za Shirikisho (CFR) Sehemu ya 300 yanaweza kupatikana kwenye [Sajili ya Shirikisho](#)).

Unastahiki haki za mzazi ikiwa wewe ni:

- mzazi kibiolojia au mzazi wa kupanga
- mlezi (Tafadhali zingatia kuwa iwapo mtoto yumo katika uangalizi wa Idara ya Watoto na Familia ya Vermont (DCF), jimbo haliwezi kuwa mlezi wa mtoto huyo.)
- mtu ambaye anachukua nafasi ya mzazi, kama vile nyanya au babu au mzazi wa kambo ambaye anaishi na mtoto huyo na ambaye anamwajibikia mtoto huyo kisheria
- mzazi ambaye ameteuliwa na [Mpango wa Vermont wa Mzazi Msaidizi wa Kielimu](#) kwa mujibu wa VTSBE 2368; 34 CFR Sehemu ya 300.519
- mzazi mlezi ambaye ameteuliwa kuwa mzazi msaidizi wa kielimu

Lazima upokee nakala ya haki zako kutoka kwa shule ya mtoto wako wakati:

- tathmini ya awali au tathmini mpya ya mtoto wako inapangwa; au
- wewe au shule hiyo itaomba kikao cha mchakato faafu; au
- utaandikisha malalamishi ya kiutawala; au
- ukiomba; au
- angalau kwa mwaka

Haki muhimu zaidi ya elimu maalum inakuhakikishia:

- kufahamishwa juu ya maamuzi muhimu yanayohusu elimu ya mtoto wako
- kutoa kibali chako kabla ya mtoto wako kufanyiwa tathmini, kabla mtoto wako hajapokea elimu maalum na huduma zinazohusiana, na kabla ya taarifa za siri kuhusu mtoto wako hazijatolewa
- kushiriki katika mikutano inayohusu tathmini ya mtoto wako, ustahiki wa elimu maalum, mipango ya kielimu, na nafasi yake
- kufikia rekodi za elimu ya mtoto wako na kufanya rekodi hizo kuwekwa siri
- kukata rufaa dhidi ya maamuzi ambayo hukubaliani nayo

Mchango wa Mzazi katika Kanuni za Elimu Maalum za Vermont

Kukuza na kupitia Mpango wa Elimu wa Mtu Binafsi (IEP) ya mtoto kunajumuisha mchango wa mzazi katika mchakato wote, ikiwemo mchango mahususi kuhusiana na viwango vya sasa vya utendaji wa mtoto wao kielimu na kiutendaji. Mchango wa mzazi unajumuishwa kupitia Sehemu ya Mchango wa Mzazi au Ukurasa uliopo kwenye IEP au kama kiambatisho kupitia Fomu ya Mchango wa Mzazi (Fomu #12 au njia nyingine ya kukusanya mchango wa Mzazi) ikiwa na taarifa inayorejelea Fomu ndani ya nyaraka ya IEP. Fomu ya Mchango wa Mzazi inakuwa sehemu ya faili ya mwanafunzi. Wazazi wanaotoa mchango katika maandishi wana haki ya kujaza na kutumia timu ya IEP ndani ya siku kumi (10) baada ya kupokea IEP husika, ikiwa ni baada ya mkutano wa IEP kufanyika ili kuandika au kurekebisha IEP. M(wa)zazi atafahamishwa kurejesha fomu hiyo (au njia nyingine ya kukusanya Mchango wa Mzazi) ndani ya siku 10 ikiwa ana mrejesho au mchango zaidi.

Inafaa na inahimizwa kwa wazazi kutoa mchango kwa kusema wakati wa mkutano wa IEP, ili wilaya iujumuishe kwenye IEP iliyoandikwa. Ukurasa wa Mchango wa Mzazi ulioelezwa hapo juu unatoa mbinu nyingine kwa wazazi kutoa mchango wao, lakini hii haipaswi kufasiliwa kama kuzuia kurekodiwa kwa mchango katika usemi. Zaidi ya hayo, wazazi wanaweza kuacha haki yao ya kutoa mchango wa mzazi ikiwa wataamua wenyewe. Ikiwa wazazi husika watakataa au hawatatoa mrejesho, LEA inapaswa kuonyesha hali hii ndani ya sehemu ya Mchango wa Mzazi katika IEP.

IEP itachukuliwa 'kuanza kutumika' kutoka tarehe inayorejelewa kama tarehe ya utekelezaji kwenye Notisi ya Awali katika Maandishi. Mkutano wa baadaye wa kukagua mchango ambao unarekebisha IEP, ikiwa utafanyika, utasababisha IEP na Notisi ya Awali katika Maandishi mpya.

Ikiwa mzazi atatofautiana na Timu ya IEP au kutoa mchango mpya ambao unaibua umuhimu wa majadiliano zaidi ya Timu ya IEP, LEA inapaswa kuandaa mkutano wa ziada iwapo yaliyomo katika mrejesho wa mzazi yanahitaji kikao kama hicho. Hii aghalabu itachukua mfumo wa taarifa mpya ambayo haijashughulikiwa tayari katika mkutano wa IEP, au shauku kuhusu mchakato wa IEP ambazo zinahitaji kushughulikiwa. Katika hali hii LEA itathibitisha kupokea mrejesho huo na inaweza ama kupanga mkutano rasmi wa ziada wa IEP kwa timu ya IEP kudhukuru mchango uliotolewa, au mkutano mahususi na msimamizi wa kesi au msimamizi wa elimu maalum. LEA inapaswa kupanga mkutano kamili wa IEP ikiwa mzazi ataomba. Marekebisho yoyote yanaweza kuandaliwa kwa kutumia fomu 5B, kama ilivyo kawaida kwa mchakato wa kurekebisha IEP baina ya mikutano ya kila mwaka.

Mchango wa Mzazi katika maudhui kwenye IEP

Dondoo kutoka kwenye Kanuni ya 2363.7 ya Elimu Maalum Maudhui ya IEP (34 C.F.R. § 300.320):

(j) Mchango wa Mzazi. IEP itajumuisha sehemu ya wazazi kutoa maoni katika maandishi kuhusu IEP ya watoto wao. Kufuatia mkutano wa IEP wa kuandika au kurekebisha IEP fulani, LEA itatuma IEP hiyo kwa mzazi pamoja na Notisi ya awali katika maandishi ya uamuzi. Mzazi atapewa siku 10 za kujaza na kurejesha sehemu ya mchango wa mzazi kwenye IEP. Azma ya sehemu ya mchango wa mzazi ni kuwezesha mrejesho kutoka kwa familia ili kuhakikisha kwamba wanapewa fursa ya kueleza maoni yao kuhusu IEP au mchakato wa IEP. Baada ya kupokea mchango wa mzazi, LEA inaweza, lakini haihitajiki kufanya hivyo, kupanga mkutano kujadili shauku za mzazi.

Taarifa ya Jumla

Notisi ya Awali katika Maandishi

Notisi

Wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima ukupe notisi katika maandishi (maelezo katika maandishi), wakati wowote:

1. Inapopendekeza kuanza au kubadilisha utambulisho, tathmini, au nafasi ya kielimu ya mtoto wako, au utoaji wa elimu faafu ya umma bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako; au
2. Inapokataa kuanza au kubadilisha utambulisho, tathmini au nafasi ya kielimu ya mtoto wako au utoaji wa FAPE kwa mtoto wako; au
3. Haijakamilisha tathmini ya awali au kuitisha mkutano wa tathmini ndani ya siku 15 za kupokea rufaa; au
4. Inakabiliana na ucheleweshwaji katika kukamilisha tathmini ya awali kwa zaidi ya siku 60, kukiwa na maelezo yanayobainisha tarehe inayotazamiwa kukamilishwa

Kanuni 2365.1.1; 2362.2.1; 34 CFR §300.503; §300.306

Yaliyomo kwenye notisi

Notisi iliyoandikwa lazima:

1. Ieleze hatua ambazo wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi unapendekeza au unakataa kuchukua
2. Ieleze kwa nini wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi unapendekeza au kukataa kuchukua hatua hiyo
3. Ieleze kila utaratibu wa tathmini, rekodi, au ripoti ambayo wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi ulitumia katika kuamua kupendekeza au kukataa hatua husika
4. Ijumuishe taarifa kwamba umelindwa kwa mujibu wa maelezo ya ulinzi wa kiutaratibu katika Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont
5. Ieueze jinsi unavyoweza kupata maelezo ya ulinzi wa kiutaratibu ikiwa hatua ambayo wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi unapendekeza au kukataa sio rufaa au tathmini ya awali
6. Ijumuishe nyenzo ambazo unaweza kuwasiliana nazo ili upate msaada katika kuelewa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont
7. Ieleze chaguzi nyingine zozote ambazo Timu ya mpango wa elimu wa mtu binafsi (IEP) ya mtoto wako ilizingatia na sababu za chaguzi hizo kukataliwa; na
8. Itoe maelezo ya sababu nyingine kwa nini wilaya ya shule ya mtoto wako au muungano wa usimamizi ulipendekeza au kukataa hatua husika

Notisi katika lugha inayoeleweka

Notisi lazima:

1. Inadikwe katika lugha inayoeleweka na umma kwa jumla; na
2. Itolewe katika lugha yako ya asili au njia nyingine ya mawasiliano unayotumia, isipokuwa kama haiwezekani kufanya hivyo

Ikiwa lugha yako ya asili au njia nyingine ya mawasiliano haiko katika maandishi, wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi lazima uhakikishe kwamba:

1. Notisi imetafsiriwa kwako kwa mdomo kupitia kwa njia nyingine katika lugha yako ya asili au njia nyingine ya mawasiliano
2. Unaelewa yaliyomo katika notisi hiyo; na
3. Kuna ushahidi katika maandishi kuwa mahitaji ya 1 na 2 yametimizwa

Lugha ya Asili

Lugha ya asili, inapotumika kwa mtu ambaye anafahamu kiingereza kidogo, ina maana ifuatayo:

1. Lugha ambayo mtu huyo hutumia kwa kawaida, au, katika hali ya mtoto, lugha ambayo inatumika kwa kawaida na wazazi wa mtoto huyo
2. Lugha inayotumika kwa kawaida na mtoto katika mazingira ya nyumbani au ya kujifunza

Kwa mtu aliye kiziwi au kipofu, au kwa mtu ambaye hana lugha iliyo katika maandishi, njia ya mawasiliano ni ile ambayo mtu huyo hutumia kwa kawaida (kama vile lugha ishara, Breli, au mawasiliano kwa njia ya mdomo).

34 CFR §300.29

Barua Pepe

Ikiwa wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi unatoa chaguzi za wazazi kupokea nyaraka kupitia barua pepe, unaweza kuchagua kupokea nyaraka zifuatazo kwa barua pepe:

1. Notisi ya awali katika maandishi
2. Notisi ya ulinzi wa kiutaratibu; na
3. Notisi zinazohusiana na malalamishi kuhusu mchakato faafu

Kanuni 2365.1.1(h) (4); 34 CFR §300.505

Kibali cha Mzazi - Ufasili

Kibali inamaanisha:

1. Umefahamishwa kikamilifu katika lugha yako ya asili au njia nyingine ya mawasiliano (kama vile lugha ishara, Breli, au mawasiliano kwa njia ya mdomo) kuhusu taarifa zote zinazohusiana na hatua ambayo unatoa kibali.
2. Unaelewa na kukubaliana katika maandishi na hatua hiyo, na kibali kinaeleza hatua hiyo na kuorodhesha rekodi (ikiwa zipo) ambazo zitatolewa na kwa nani; na:
3. Unaelewa kwamba kibali ni cha hiari kwa upande wako na kwamba unaweza kubatilisha kibali chako wakati wowote.

Kubatilisha kibali chako hakukanushi (kutendua) hatua ambayo imetendeka baada ya kutoa kibali na kabla ya kukibatilisha.

Kanuni 2365.1.3; 34 CFR §300.9

Kibali cha Mzazi

Tazama [34 CFR §300.300](#) kwa maelezo kuhusiana na kibali cha mzazi.

Kibali kwa tathmini ya awali

Wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi hauwezi kuendesha tathmini ya awali kwa mtoto wako kuamua iwapo mtoto wako anastahiki kwa mujibu wa sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont bila ya kwanza kukupatia Notisi ya awali katika maandishi kuhusu hatua inayopendekezwa na bila kupata kibali chako kama ilivyoelezwa katika nyaraka hii kwenye anwani Kibali cha Mzazi.

Wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi lazima utie juhudi kadri inavyoweze kupata kibali chako kwa tathmini ya awali kuamua iwapo mtoto wako ni mtoto mwenye ulemavu.

Kibali chako kwa tathmini ya awali haimaanishi kwamba pia umetoa kibali kwa wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi kuanza kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mtoto wako.

Ikiwa mtoto wako amesajiliwa katika shule ya umma au unataka kumsajili mtoto wako katika shule ya umma na umekataa kutoa kibali au kukosa kujibu maombi ya kutoa kibali kwa tathmini ya awali, wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi unaweza, lakini hawahitajiki kufanya hivyo, kujaribu kufanya tathmini ya awali kwa kutumia upatanishi, kufuata mchakato faafu, au kukagua data iliyoko. Wilaya ya shule/muungano wa usimamizi unaweza kuamua kutofuata tathmini hiyo na watarekodi sababu za kufanya hivyo katika rekodi ya mtoto wako. Wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi hautakiuka wajibu wake wa kutafuta, kutambua na kutathmini mtoto wako ikiwa hautafuatilia tathmini ambayo mzazi amekataa kutoa kibali.

Kanuni maalum kwa tathmini ya awali ya Watoto walio chini ya ulinzi wa Serikali

Kuhusiana na mtoto ambaye yumo chini ya ulinzi wa Serikali na haishi na mzazi wake, wilaya ya shule haihitaji kibali kutoka kwa mzazi kwa ajili ya tathmini ya awali ili kubaini iwapo mtoto huyo ni mtoto mwenye ulemavu ikiwa:

1. Licha ya juhudi zinazofaa za kufanya hivyo, wilaya ya shule haiwezi kumpata mzazi wa mtoto huyo.
2. Haki za mzazi zimekatishwa kwa mujibu wa Sheria za Jimbo; au:
3. Jaji ametoa haki za kufanya maamuzi ya kielimu na kibali kwa tathmini ya awali kwa mtu mwingine kando na mzazi huyo.

Watoto walio chini ya ulinzi wa Serikali, kama inavyotumiwa katika IDEA, inarejela mtoto ambaye, kama ilivyobainishwa na Jimbo ambapo mtoto huyo anaishi, ni:

1. Mtoto wa kulea
2. Anachukuliwa kuwa mtoto aliye chini ya ulinzi wa Serikali kwa mujibu wa sheria za Jimbo; au
3. Yumo chini ya uangalizi wa wakala wa umma wa ustawi wa watoto

Mtoto aliye chini ya ulinzi wa Serikali haijumuishi mtoto wa kulea aliye na mzazi mlezi.

Kibali cha mzazi kwa huduma

Wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi lazima upate kibali kabla ya kuanza kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mtoto wako kwa mara ya kwanza na lazima watie juhudu zinazofaa kupata kibali chako.

Ikiwa hutajibu maombi ya kibali chako kwa mtoto wako kupokea elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mara ya kwanza, au ikiwa utakataa kutoa kibali hicho, wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi unaweza kutumia ulinzi wa kiutaratibu (k.v. Upatanishi, malalamishi ya mchakato faafu, mkutano wa kusuluhisha, au kikao cha mchakato faafu kisichokuwa na upendeleo) ili kupata makubaliano au uamuzi kwamba elimu maalum na huduma zinazohusiana (zilizopendekezwa na Timu ya IEP ya mtoto wako) zinaweza kutolewa kwa mtoto wako bila kibali chako.

Ikiwa utakataa kutoa kibali chako kwa mtoto wako kupokea elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mara ya kwanza, au ikiwa hautajibu maombi ya kutoa kibali hicho na wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi ukakosa kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mtoto wako ambazo waliomba kibali chako, wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi:

1. Hawakiuki mahitaji ya kuhakikisha elimu faafu ya umma bila malipo (FAPE) inapatikana kwa mtoto wako kwa kukosa kutoa huduma hizo kwa mtoto wako; na:
2. Hawahitajiki kuwa na mkutano wa mpango wa elimu wa mtu binafsi (IEP) au kuandaa IEP kwa mtoto wako kwa elimu maalum na huduma zinazohusiana ambazo waliomba kibali chako.

Kubatilisha kibali cha mzazi kwa huduma

Una haki ya kubatilisha kibali chako kwa huduma za elimu maalum wakati wowote kabla au baada ya huduma hizo kuanza.

Ikiwa utafanya hivyo, wilaya ya shule au muungano wa usimamizi hauwezi kuomba upatanishi au kikao cha mchakato faafu.

Zaidi ya hayo, mtoto wako hatakuwa amelindwa kuhusiana na nidhamu kwa mujibu wa kanuni za elimu maalum.

Ikiwa utabatilisha kibali chako, mtoto wako bado anaweza kulindwa dhidi ya ubaguzi kwa mujibu wa Kifungu cha 504 cha Sheria ya Urekebishaji ya 1973 na unaweza kuomba kwamba shule izingatie manufaa ambayo mtoto wako huenda anastahiki kwa mujibu wa Kifungu cha 504.

Kibali cha mzazi kwa tathmini mpya

Wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi lazima upate kibali chako kabla ya kufanya tathmini mpya kwa mtoto wako, isipokuwa kama wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi unaweza kudhihirisha kuwa

1. Ulichukua hatua zinazofaa kupata kibali chako kwa tathmini mpya ya mtoto wako; na
2. Wewe haukujibu

Ikiwa utakataa kutoa kibali kwa tathmini mpya ya mtoto wako, wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi unaweza, lakini hauhitajiki, kufuatilia tathmini mpya ya mtoto wako kwa kutumia upatanishi, malalamishi ya mchakato faafu, mkutano wa kusuluhisha, na kikao cha mchakato faafu kisichokuwa na upendeleo kutafuta kubatilisha kukataa kwako kuridhia tathmini mpya kwa mtoto wako. Kama ilivyo kwa tathmini, wilaya ya shule yako haitakuwa imekiuka wajibu wake kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA iwapo itakataa kufuatilia tathmini mpya kwa njia hii.

Rekodi za juhudi faafu za kupata kibali cha mzazi

Shule yako lazima iweke rekodi zake za juhudi faafu za kupata kibali cha mzazi kibali kwa tathmini ya awali, ili kutoa elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mara ya kwanza, kufanya tathmini mpya na kutafuta wazazi wa watoto walio chini ya ulinzi wa serikali kwa tathmini ya awali. Rekodi hizo lazima zijumuishe rekodi ya juhudi za wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi katika masuala haya, kama vile:

1. Rekodi za kina za simu zilizopigwa au majaribio ya kupiga simu na matokeo ya simu hizo;
2. Nakala za barua zilizotumwa kwa wazazi na majibu yoyote yaliyopokelewa; na
3. Rekodi za kina za ziara zilizofanywa nyumbani kwako au mahali pa ajira na matokeo ya ziara hizo.

Mahitaji mengine ya kibali

Kibali chako hakihitajiki kabla wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi:

1. Haujakagua data iliyopo kama sehemu ya tathmini ya mtoto wako au tathmini mpya; au
2. Haujampa mtoto wako jaribio au tathmini nyingine ambayo inatolewa kwa watoto wote isipokuwa kama, kabla ya jaribio hilo au tathmini, kibali kinahitajika kutoka kwa wazazi wote wa watoto wote

Wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi haupaswi kutumia kukataa kwako kutoa kibali kwa huduma moja au shughuli kukunyima au kumnyima mtoto wako huduma, manufaa au shughuli nyingine.

Ikiwa umemsajili mtoto wako katika shule ya kibinafsi kwa gharama yako mwenyewe au unamwelimisha mtoto wako kutoka nyumbani, na hautoi kibali chako kwa tathmini ya awali kwa mtoto wako au tathmini mpya kwa mtoto wako, au hautaki kujibu ombi la kutoa kibali chako, wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi hauwezi kutumia upatanishi, malalamishi ya mchakato faafu, mkutano wa kusuluhisha, au kikao cha mchakato faafu kisichokuwa na upendeleo kutafuta kubatilisha kukataa kwako kuridhia, na haihitajiki ili kuzingatia mtoto wako kuwa anastahiki kupokea huduma sawa (huduma zinazotolewa kwa watoto walio na ulemavu na waliosajiliwa na wazazi katika shule ya kibinafsi).

Tathmini Huru za Kielimu

Kanuni 2362.2.8; 34 CFR §300.502

Jumla

Kama ilivyoelezwa hapa hapa chini, una haki ya kupata tathmini huru ya kielimu (IEE) kwa mtoto wako ikiwa unatofautiana na tathmini ya mtoto wako ambayo ilifanywa na wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi.

Ikiwa utaomba IEE, wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi lazima ukupatie taarifa kuhusu mahali ambapo unaweza kupata IEE na kuhusu vigezo vya wilaya ya shule au vya muungano wa usimamizi vinavyotumika kwa IEE.

Ufasili

Tathmini Huru ya Kielimu inamaanisha tathmini inayoendeshwa na mtahini aliyehitimu ambaye si mwajiriwa wa wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi unaowajibika kwa elimu ya mtoto wako.

Gharama ya umma inamaanisha kwamba wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi ama unalipia gharama zote za tathmini au unahakikisha kwamba tathmini inatolewa bila ya gharama zozote kwako.

Haki ya mzazi ya tathmini kwa gharama ya umma

Una haki ya kupata tathmini huru ya kielimu kwa mtoto wako kwa gharama ya umma ikiwa unatofautiana na tathmini ya mtoto wako ambayo ilifanywa na wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi, kwa kuzingatia masharti yafuatayo:

1. Ikiwa utaomba tathmini huru ya kielimu kwa mtoto wako kwa gharama ya umma, wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi lazima, bila kuchelewesha, ama: (a) Kuwasilisha malalamishi ya mchakato faafu kuomba kikao cha kuonyesha kwamba tathmini yake ya mtoto wako ni faafu; au (b) Kutoa tathmini huru ya kielimu kwa gharama ya umma, isipokuwa kama wilaya ya shule au muungano wa usimamizi utaonyesha katika kikao kuwa tathmini ya mtoto wako uliyopata haikukidhi vigezo vya wilaya ya shule.
2. Ikiwa wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi utaomba kikao na uamuzi wa mwisho ni kwamba tathmini ya wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi kwa mtoto wako ni faafu, bado una haki ya kupata tathmini huru ya kielimu, lakini sio kwa gharama ya umma.
3. Ikiwa utaomba tathmini huru ya kielimu kwa mtoto wako, wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi unaweza kuuliza kwa nini unapinga tathmini ya mtoto wako kutolewa na wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi. Hata hivyo, wilaya ya shule yako au muungano wa wilaya hauwezi kukuhitaji kutoa maelezo na hauwezi kuchelewesha ama kutoa tathmini huru ya kielimu ya mtoto wako kwa gharama ya umma au kuwasilisha malalamishi ya mchakato faafu ili kuomba kikao cha mchakato faafu kutetea tathmini ya wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi kwa mtoto wako.

Una haki ya tathmini moja huru ya kielimu kwa mtoto wako kwa gharama ya umma kila mara wilaya ya shule yako au muungano wa ulinzi utaendesha tathmini ya mtoto wako ambayo unatofautiana nayo.

Tathmini zinazoanzishwa na Mzazi

Ikiwa utapata tathmini huru ya kielimu kwa mtoto wako kwa gharama ya umma au utashiriki tathmini ya mtoto wako uliyopata kwa gharama ya kibinafsi na wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi:

1. Wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi lazima uzingatie matokeo ya tathmini ya mtoto wako, ikiwa inatimiza vigezo vya wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi kwa tathmini huru za kielimu, katika uamuzi wowote utakaofanywa kuhusu utoaji wa elimu faafu ya umma bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako; na
2. Wewe au wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi unaweza kuwasilisha tathmini hiyo kama ushahidi katika kikao cha mchakato faafu kuhusu mtoto wako.

Maombi ya tathmini ya Maafisa waamuzi

Ikiwa afisa mwamuzi ataomba tathmini huru ya kielimu kwa mtoto wako kama sehemu ya kikao cha mchakato faafu, gharama ya tathmini hiyo lazima iwe gharama ya umma.

Vigezo vya wilaya ya shule/muongano wa usimamizi

Ikiwa tathmini huru ya kielimu ni kwa gharama ya umma, vigezo vya upataji wa tathmini hiyo, ikiwemo eneo la tathmini na kiwango cha kuhitimu cha anayefanya tathmini, lazima viwe sawa na vigezo ambavyo wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi hutumia unapoanzisha tathmini. Isipokuwa vigezo vilivyoelezwa hapo juu, wilaya ya shule au muungano wa usimamizi hauwezi kuweka masharti au makataa yanayohusiana na upataji tathmini huru ya kielimu kwa gharama ya umma.

Usiri wa Taarifa

Ufasili

Kama ilivyotumiwa chini ya anwani ya Usiri wa Taarifa:

- Uharibifu unamaanisha uharibifu halisi au kuondolewa kwa vitambulisho vya kibinafsi kutoka kwa taarifa ili maelezo yasitambulike tena kibinafsi.
- Rekodi za elimu inamaanisha aina ya rekodi zinazorejelewa kwenye ufasili wa “rekodi za elimu” katika 34 CFR Sehemu ya 99 (masharti ya utekelezaji wa Sheria ya Haki za Kielimu kwa Familia na Faragha ya 1974, 20 U.S.C. 1232g (FERPA)).
- Wakala mshiriki inamaanisha wilaya ya shule au muungano wowote wa usimamizi, wakala au asasi inayokusanya, kuhifadhi, au kutumia taarifa inayoweza kumtambulisha mtu binafsi, au ambayo taarifa zinapatikana kwake, kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont.

Kanuni 2365.2 34; CFR §300.611

Inayomtambulisha Mtu Binafsi

Inayomtambulisha Mtu Binafsi inamaanisha taarifa ambayo iko na:

- Jina la mtoto wako, jina lako kama mzazi, au jina la mtu mwingine wa familia;
- Anwani ya mtoto wako;
- Kitambulisho cha kibinafsi, kama vile nambari ya usalama wa kijamii ya mtoto wako au nambari ya mwanafunzi; au
- Orodha ya sifa za kibinafsi au taarifa nyingine ambayo inaweza kutumiwa kumtambua mtoto wako kwa uhakika.

34 CFR §300.32

Notisi kwa Wazazi

Wakala wa Elimu wa Vermont lazima watoe notisi ambayo inatosha kuwafahamisha wazazi kikamilifu kuhusu usiri wa taarifa inayomtambulisha mtu binafsi, ikiwemo:

1. Maelezo ya kiwango ambacho notisi inatolewa katika lugha ya asili ya watu wa makundi tofauti katika Jimbo;
2. Maelezo ya watoto ambao taarifa yao inayomtambulisha mtu binafsi inahifadhiwa, aina ya taarifa inayotafutwa, mbinu ambazo jimbo linapanga kutumia katika kukusanya taarifa hiyo (ikiwemo vyanzo ambapo watapata taarifa hii), na matumizi ya taarifa husika;
3. Muhtasari wa sera na taratibu ambazo asasi zinazoshiriki lazima zifuate kuhusiana na uhifadhi, ufichuzi kwa mhusika wa tatu, uzuiaji, na uharibifu wa taarifa inayomtambulisha mtu binafsi; na:
4. Maelezo ya haki zote za wazazi na watoto kuhusiana na taarifa hii, ikiwemo haki kwa mujibu wa Sheria ya Haki za Kielimu kwa Familia na Faragha (FERPA) na utekelezaji wa masharti katika kifungu cha 34 CFR Sehemu ya 99.

Kabla ya utambulisho wowote mkuu, upataji, au shughuli ya tathmini (pia inajulikana kama “kupata mtoto”), notisi lazima ichapishwe au kutangazwa katika magazeti au vyombo vingine vya habari, au njia zote mbili, zenye msambao wa kutosha kuwafahamisha wazazi wote katika Jimbo lote kuhusu shughuli ya kupata, kutambua na kutathmini watoto wanaohitaji elimu maalum na huduma zinazohusiana.

Kanuni 2365.2.1; 34 CFR §300.612

Haki za ufikiaji

Wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi lazima ukuruhusu kukagua na kupitia rekodi zozote za elimu zinazohusiana na mtoto wako ambazo zilikusanywa, kuhifadhiwa, au kutumiwa na wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na masharti ya jimbo kuhusu elimu maalum. Wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima uridhie maombi yako ya kukagua na kupitia rekodi zozote za elimu kuhusu mtoto wako bila kuchelewesha na kabla ya mkutano wowote unaohusu mpango wa elimu wa mtu binafsi (IEP), au kikao cha mchakato faafu kisichokuwa na upendeleo (ikiwemo mkutano wa kusuluhisha au kikao kuhusu nidhamu), na haipaswi kuzidi siku 45 za kalenda baada ya wewe kuomba.

Haki yako ya kukagua na kupitia rekodi za elimu inajumuisha:

1. Haki yako ya kupata majibu kutoka kwa wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi kwa maombi yako ya kupata maelezo na ufafanuzi wa rekodi hizo;

2. Haki yako ya kuomba wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi kukupa nakala za rekodi hizo ikiwa huwezi kuzikagua na kuzipitia ipasavyo kama hujapokea nakala hizo; na:
3. Haki yako ya kumwezesha mwakilishi wako kukagua na kupitia rekodi hizo.

Wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi unaweza kuchukulia kwamba una mamlaka ya kukagua na kupitia rekodi zinazomhusu mtoto wako isipokuwa kama wataelezwa kuwa huna mamlaka kwa mujibu wa sheria za Jimbo zinazodhibiti masuala kama vile ulezi, kutengana na/au talaka.

Kanuni 2365.2.2; 34 CFR §300.613

Rekodi ya Ufikiaji

Kila wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima uweke rekodi ya wadau wanaofikia rekodi za elimu zilizokusanywa, kuhifadhiwa, au kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na masharti ya jimbo kuhusu elimu maalum (isipokuwa ufikiaji wa mzazi na wafanyakazi walioruhusiwa na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi), ikiwemo jina la mdau, tarehe ufikiaji ulipotolewa, na azma ya mdau kuruhusiwa kutumia rekodi hizo.

Kanuni 2365.2.3; 34 CFR §300.614

Rekodi kuhusu Zaidi ya Mtoto Mmoja

Ikiwa rekodi zozote za elimu zinajumuisha taarifa kuhusu zaidi ya mtoto mmoja, wazazi wa watoto hao wana haki ya kukagua na kupitia taarifa inayohusiana na watoto wao pekee au kufahamishwa kuhusu taarifa hiyo mahususi.

Kanuni 2365.2.4 34; CFR §300.615

Orodha ya Aina na Maeneo ya Taarifa

Baada ya maombi, kila wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima ukupatie orodha ya aina na maeneo ambapo rekodi zinakusanywa, kuhifadhiwa, au kutumiwa na wakala.

Kanuni 2365.2.5 34; CFR §300.616

Ada

Kila wilaya ya shule au muungano wa usimamizi unaweza kutoza ada kwa nakala za rekodi ambazo umetengenezewa kwa mujibu wa masharti ya shirikisho na ya jimbo kuhusu elimu maalum ikiwa ada hiyo haikuzi katika kutekeleza haki yako ya kukagua na kupitia rekodi hizo.

Wilaya ya shule au muungano wa usimamizi hauwezi kutoza ada za kutafuta au kupata taarifa kwa mujibu wa masharti haya.

Kanuni 2365.2.6 34; CFR §300.617

Marekebisho ya Rekodi kutokana na Ombi la Mzazi

Iwapo unaamini kwamba taarifa katika rekodi za elimu zilizokusanywa kuhusu mtoto wako, kuhifadhiwa, au kutumiwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na masharti ya Jimbo kuhusu elimu maalum si sahihi, zinapotosha, au zinakiuka faragha au haki nyingine za mtoto wako, unaweza kuomba wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ambao unatunza taarifa hiyo kuibadilisha.

Wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima uamue iwapo utabadilisha taarifa hiyo kuambatana na ombi lako ndani ya kipindi faafu baada ya kupokea ombi hilo.

Ikiwa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi utakataa kubadilisha taarifa kulingana na ombi lako, lazima wakueleze kuhusu kukataa huko na wakushauri kuhusu haki yako ya kusikizwa kwa ajili hii kama ilivyoelezwa hapa chini kwenye anwani ya *Fursa ya kikao cha kusikilizwa*.

Kanuni 2365.2.7 34; CFR §300.618

Fursa ya Kikao cha Kusikilizwa

Wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima, baada ya ombi, utoe fursa ya kikao cha kusikilizwa kuhoji taarifa katika rekodi za elimu kuhusiana na mtoto wako ili kuhakikisha kwamba ni sahihi, haipotoshi, au vinginevyo haikiuki faragha na haki nyingine za mtoto wako.

Kanuni 2365.2.8; 34 CFR §300.619

Utaratibu wa Kikao cha kusikilizwa

Kiako cha kuhoji taarifa katika rekodi za elimu lazima kiendeshwe kulingana na taratibu za vikao kama hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Haki za Kielimu kwa Familia na Faragha (FERPA).

34 CFR §300.621

Matokeo ya Kikao

Ikiwa, kutokana na kikao cha kusikilizwa, wilaya ya shule au muungano wa usimamizi utaamua kwamba taarifa hiyo si sahihi, inapotosha, au vinginevyo inakiuka faragha au haki nyingine za mtoto, lazima wabadilishe taarifa ipasavyo na kukufahamisha katika maandishi.

Ikiwa, kutokana na kikao cha kusikilizwa, wilaya ya shule au muungano wa usimamizi utaamua kwamba taarifa hiyo ni sahihi, haipotoshi, au vinginevyo haikiuki faragha au haki nyingine za mtoto wako, lazima wakufahamishe kuhusu haki yako ya kuweka katika rekodi ambazo wanahifadhi kuhusu mtoto wako, habari kuhusu taarifa au kutoa sababu za kukosa kukubaliana na uamuzi wa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi.

Maelezo kama haya yanayowekwa katika rekodi za mtoto wako lazima:

1. Yahifadhiwe na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi kama sehemu ya rekodi za mtoto wako kwa muda ambao rekodi hiyo au sehemu iliyokuwa na utata itahifadhiwa na wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi; na:
2. Iwapo wialaya ya shule au muungano wa usimamizi utafichua kwamba rekodi za mtoto wako au sehemu iliyokuwa na utata kwa mhusika yeyote, maelezo hayo pia lazima yafichuliwe kwa mdau huyo.

Kanuni 2365.2.9; 34 CFR §300.620

Kibali cha Ufichuzi wa Taarifa Inayomtambulisha Mtu Binafsi

Isipokuwa kwa ufichuzi ambao unaruhusiwa kwa maafisa wa polisi na wa mahakama ambapo kibali cha mzazi hakihitajiki kwa Sheria ya Haki za Kielimu kwa Familia na Faragha (FERPA), lazima utoe kibali chako kabla taarifa inayomtambulisha mtu binafsi haijafichuliwa kwa wadau kando na maafisa au asasi zinazoshiriki. Isopokuwa katika hali zilizoenezwa hapa chini, kibali chako hakihitajiki kabla ya taarifa inayomtambulisha mtu binafsi haijatolewa kwa maafisa wa mashirika yanayoshiriki kwa ajili ya kutimiza mahitaji ya Sehemu B ya IDEA na masharti ya jimbo kuhusu elimu maalum.

Kibali chako, au kibali cha mtoto anayestahiki ambaye amefikia umri wa kuwa mtu mzima kwa mujibu wa sheria za Jimbo, lazima kipatikane kabla ya taarifa inayomtambulisha mtu binafsi kutolewa kwa maafisa wa mashirika yanayoshiriki kutoa au kulipia huduma za mpito.

Ikiwa mtoto wako yuko, au ataenda, katika shule ya kibinafsi ambayo haipo katika eneo sawa la wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ambapo unaishi, kibali chako lazima kipatikane kabla taarifa yoyote inayomtambulisha mtu binafsi kuhusu mtoto wako kuachiliwa baina ya maafisa katika wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ambapo shule hiyo huru inapatikana na maafisa katika wilaya ya shule au muungano wa usimamizi wa mahali unapoishi.

Kanuni 2365.2.11; 34 CFR §300.622

Ulinzi

Kila wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima ulinde usiri wa taarifa inayomtambulisha mtu binafsi katika hatua za ukusanyaji, uhifadhi, ufichuzi na uharibifu.

Afisa mmoja katika wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi lazima achukue jukumu la kuhakikisha usiri wa taarifa yoyote inayomtambulisha mtu binafsi.

Kila wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima uwe na sera au taratibu za kuhakikisha kwamba watu wote wanaokusanya au kutumia taarifa inayomtambulisha mtu binafsi wanapokea mafunzo au maagizo kuhusu sera na taratibu za Vermont kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, Kanuni ya 2365.2.12 na Sheria ya Haki za Kielimu kwa Familia na Faragha (FERPA).

Kila wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima uhifadhi, kwa ukaguzi wa umma, orodha ya sasa ya majina na wadhifa wa wafanyakazi katika shirika ambao wanaweza kufikia taarifa inayomtambulisha mtu binafsi.

Kanuni 2365.2.12; 34 CFR §300.623

Uharibifu wa Taarifa

Wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi lazima ukufahamishe wakati taarifa inayomtambulisha mtu binafsi iliyokusanywa, kuhifadhiwa, au kutumiwa haihitajiki tena katika kutoa huduma za kielimu kwa mtoto wako.

Taarifa hiyo lazima iharibiwe pindi ukiomba. Hata hivyo, rekodi ya kudumu ya jina la mtoto wako, anwani na nambari ya simu, alama zake, rekodi ya mahudhurio, madarasa aliyohudhuria, madarasa aliyokamilisha, na mwaka alipokamilisha inaweza kuhifadhiwa bila kikomo cha muda.

Kanuni 2365.2.13; 34 CFR §300.624

Taratibu za Malalamishi za Vermont

Tofauti kati ya Kikao cha Malalamishi kuhusu Mchakato Faafu na Taratibu za Malalamishi ya Kiutawala

Masharti ya Sehemu B ya IDEA na Sheria za Elimu Maalum za Vermont zinaeleza taratibu tofauti kwa malalamishi ya kiutawala na vikao na malalamishi ya mchakato faafu. Kama ilivyoelezwa hapa chini, mtu au shirika lolote linaweza kuwasilisha malalamishi ya kiutawala likidai ukiukaji wa mahitaji yoyote ya Sehemu B na Sheria za Elimu Maalum za Vermont wa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi, Wakala wa Elimu wa Vermont, au shirika lingine lolote la umma. Ni wewe tu au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ndio mnaeweza kuwasilisha malalamishi ya mchakato faafu au suala lolote linalohusu pendekezo au kukataa kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini au nafasi ya kielimu ya mtoto aliye na ulemavu, au utoaji wa elimu faafu ya umma bila malipo (FAPE) kwa mtoto huyo. Ingawa Katibu wa Wakala wa Elimu wa Vermont kwa jumla lazima asuluhisha Malalamishi ya Kiutawala ndani ya kipindi cha siku 60 za kalenda, isipokuwa kama kipindi hicho kitaongezwa ipasavyo, afisa mwamuzi wa kikao cha mchakato faafu kisichokuwa na upendeleo lazima asikilize malalamishi ya mchakato faafu (ikiwa hayajasuluhishwa kupitia kwa mkutano wa kusuluhisha au kupitia kwa upatanishi) na atoe maamuzi katika maandishi ndani ya siku 45 za kalenda baada ya kuisha kwa kipindi cha kusuluhisha, kama inavyoelezwa katika nyaraka hii chini ya anwani ya Mchakato wa Kusuluhisha, isipokuwa kama afisa mwamuzi atatoa nyongeza mahususi ya kipindi kufuatia ombi lako au ombi la wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi. Malalamishi ya kiutawala na malalamishi ya mchakato faafu, taratibu za kusuluhisha na za kusikizwa zimeelezwa kwa kina zaidi hapa chini.

Taratibu za Malalamishi ya Kiutawala

34 CFR §300.151

Jumla

Malalamishi ya Kiutawala yaliyoandikwa na kutiwa sahihi lazima yaandikishwe kwa Katibu wa Wakala wa Elimu wa Vermont na nakala itumwe kwa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi au shirika la umma linalomhudumia mtoto husika.

Baada ya kupokea Malalamishi ya kiutawala, Katibu wa Elimu wa Vermont atateua mpelelezi wa malalamiko atakayeendesha uchunguzi. Mpelelezi wa malalamiko atakagua ushahidi uliowasilishwa kwa niaba ya mlalamishi na kwa niaba ya wilaya ya shule, muungano wa usimamizi au shirika lingine la umma. Kwa uamuzi wa mpelelezi wa malalamiko, malalamishi yanaweza kuchunguzwa kwa njia ya kukagua nyaraka, mkutano, kikao cha kusikizwa, uchunguzi wa nyanjani, au mseto wa njia zozote kati ya hizi.

Mpelelezi wa malalamiko atampa mlalamishi fursa ya kuwasilisha taarifa za ziada, ama kwa njia ya mdomo au kupitia maandishi, kuhusu madai yaliyomo kwenye malalamishi. Mpelelezi wa malalamiko pia anaweza kuipa wilaya ya shule, muungano wa usimamizi, au shirika lingine la umma fursa ya kujibu kukiwa na pendekezo la kusuluhisha malalamishi, au, kwa kibali chako, fursa ya kuingia katika upatanishi au mbinu mbadala za utatuzi wa migogoro.

Ikiwa kikao cha kusikizwa kitapangwa, mpelelezi wa malalamiko atakuwa na mamlaka na majukumu yaliyoelezwa hapa chini:

1. Kuendesha vikao vya kabla ya kikao cha kusikizwa;
2. Kuendesha vikao vyovyote vya kusikizwa ambavyo huenda vikahitajika;
3. Kuandaa matokeo ya ukweli yaliyopendekezwa na hitimisho la sheria kwa uamuzi wa mamlaka ya kikao cha kusikizwa; na:
4. Mamlaka na majukumu mengine yoyote yaliyobainishwa katika. Kanuni ya 1236.1 ya Bodi ya Elimu ya Jimbo.

Katibu wa Elimu wa Vermont atatoa uamuzi katika maandishi katika muda usiozidi siku 60 baada ya kupokea malalamishi.

Wakati upelelezi wa malalamishi utabaini kuwa kumekuwa na ukiukaji wa mahitaji ya shirikisho au ya jimbo kwa mujibu wa IDEA, ripoti ya uchunguzi itashughulikia jinsi ya kurekebisha ukiukaji huo, ikiwemo kunyimwa kwa huduma kulikosababishwa, ikiwa ni pamoja na, kama inavyofaa, hatua za urekebishaji zinazofaa kwa mahitaji ya mtoto, pamoja na utoaji faafu wa huduma kwa watoto wote walio na ulemavu katika siku zijazo.

Kuongeza Wakati

Ukomo wa wakati wa siku sitini za kalenda unaweza kuongezwa tu ikiwa kuna hali zisizokuwa za kawaida kuhusiana na malalamishi fulani, au ikiwa wadau watakubali kuongeza muda ili kushiriki katika upatanishi.

Malalamishi ya kiutawala na vikao vya mchakato faafu

Ikiwa malalamishi katika maandishi yatapokelewa na bado yanaangaziwa katika kikao cha mchakato faafu kama ilivyoelezwa hapa chini kwenye mada ya Kuwasilisha Malalamishi ya Mchakato Faafu, au Malalamishi ya Kiutawala yanajumuisha masuala mbalimbali, ambayo mojawapo au zaidi ni sehemu ya kikao hicho, Wakala wa Elimu wa Vermont lazima aweke kando malalamishi ya kiutawala ambayo yanashughulikiwa katika kikao cha mchakato faafu hadi kusikizwa kutakapokamilika. Suala lolote katika malalamishi ya kiutawala ambalo sio sehemu ya kikao cha mchakato faafu lazima lisuluhishwe katika ukomo wa muda na taratibu zilizoелеzwa hapo juu.

Ikiwa suala litaibuliwa katika malalamishi ambayo yameshaamuliwa hapo awali katika kikao cha mchakato faafu kilichohusisha wadau sawa, uamuzi wa kikao utafuatwa kuhusu suala hilo na Wakala wa Elimu wa Vermont lazima amfahamishe mlalamishi kwamba uamuzi huo utafuatwa.

Malalamishi yanayodai kushindwa kwa wilaya ya shule au shirika lingine la umma kutekeleza uamuzi wa kikao cha mchakato faafu lamiza yasuluhishwe na Wakala wa Elimu wa Vermont.

Kuwasilisha Malalamishi ya Kiutawala

Kanuni 2365.1.5 34 CFR§300.153

Jumla

Mtu au shirika lolote linaweza kuwasilishwa Malalamishi ya Kiutawala yaliyotiwa sahihi katika maandishi kulingana na taratibu zilizoelzwa hapo juu.

Malalamishi ya Kiutawala lazima yajumuishe:

1. Maelezo kwamba wilaya ya shule, muungano wa usimamizi au shirika lingine la umma limekiuka mahitaji ya Sehemu B ya IDEA au masharti yake;
2. Hoja ambazo ndio msingi wa maelezo hayo;
3. Sahihi na taarifa za mawasiliano za mlalamishi; na ikiwa anadai ukiukaji dhidi ya mtoto mahususi:
 - a. Jina na anwani ya makazi ya mtoto huyo;
 - b. Jina la shule ambayo mtoto anahudhuria;
 - c. Katika hali ambapo mtoto au kijana hana makazi (kwa mujibu wa maana ya kipengele cha 725(2) cha Sheria ya McKinney-Vento ya Usaidizi wa Wasiokuwa na Makazi (42 U.S.C. 11434a(2)), taarifa za mawasiliano zilizopo kwa mtoto, na jina la shule ambayo mtoto huyo anahudhuria;
 - d. Maelezo ya hali ya tatizo la mtoto huyo, ikiwemo taarifa zinazohusiana na tatizo hilo; na;
 - e. Suluhu linalopendekezwa kwa tatizo hilo kwa kiwango ambacho kinajulikana na kupatikana kwa wahusika kwa wakati ambapo malalamishi yanaandikishwa.

Isipokuwa kwa malalamishi ya kiutawala yaliyoangaziwa katika Kanuni ya 2365.1.6, malalamishi lazima yadai ukiukaji ambao ulitokea katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja (1) kutoka siku ya kupokea malalamishi yalivyoelezwa katika anwani *Taratibu za Malalamishi ya Kiutawala*.

Malalamishi ya Sehemu C

Malalamishi ya kiutawala pia yanaweza kuwasilishwa kuhusu masharti ya Sehemu C ya IDEA. Uchunguzi wa malalamishi ya Sehemu C utakamilishwa kwa ushirikiano na Shirika la Huduma za Watu, Idara ya Watoto na Familia, [Kitengo cha Maendeleo ya Watoto](#). Malalamishi katika maandishi yanapaswa kutumwa kwa [Huduma Jumuishi za Watoto](#), Kitengo cha Maendeleo ya Watoto, 280 State Drive, NOB 1 North, Waterbury, Vermont 05671-1040.

Taratibu za Malalamishi ya Mchakato Faafu

Kuwasilisha Malalamishi ya Mchakato Faafu

34 CFR §300.507

Jumla

Wewe au wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi mnaweza kuwasilisha malalamishi ya mchakato faafu kuhusu sula linalohusiana na pendekezo au kukataa kuanzisha au kubadilisha utambulisho, tathmini au nafasi ya kielimu ya mtoto wako, au utoaji wa elimu faafu ya umma bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako.

Malalamishi ya mchakato faafu lazima yadai ukiukaji ambao ulitokea katika kipindi kisichozidi miaka miwili (2) kabla ya mwasilishaji wa malalamishi kujua au alipaswa kujua kuhusu hatua inayodaiwa na inayoweka msingi wa malalamishi ya mchakato faafu. Hata hivyo, ikiwa kwa uamuzi wako binafsi umempeleka mtoto wako katika shule ya kibinafsi na unaomba urejeshaji, malalamishi ya mchakato faafu lazima yawasilishwe ndani ya siku tisini (90) tangu asajiliwe.

Ratiba iliyowekwa hapo juu haitumiki kwako ikiwa hungeweza kuwasilisja malalamishi ya mchakato faafu ndani ya ratiba hii kwa sababu:

1. Wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi ulipotosha mahususi kwamba ulikuwa umesuluhisha masuala yaliyotambuliwa katika malalamishi; au:
2. Wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi ulikataa kukupatia taarifa ambayo ulihitajika kukupa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Sheria za Elimu Maalum za Vermont.

Taarifa kwa wazazi

Wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima ukufahamisha kuhusu huduma za kisheria au huduma nyingine za bila malipo au za gharama ya chini zinazopatikana katika eneo hilo ikiwa utaomba taarifa hiyo, au ikiwa wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi utawasilisha malalamishi ya mchakato faafu.

Malalamishi ya Mchakato faafu

Kanuni 2365.1.6; 34 CFR §300.508

Jumla

Ili kuomba kikao, wewe au wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi (au wakili wako au wakili wa wilaya ya shule au wa muungano wa usimamizi) lazima awalilishe malalamishi ya mchakato faafu kwa wahusika hao wengine. Malalamishi hayo lazima yajumuishe maudhui yote yaliyoorodheshwa hapa chini na lazima yawekwe siri.

Wewe au wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi, yeyote anayewasilisha malalamishi, lazima pia atoe nakala ya malalamishi hayo kwa Wakala wa Elimu wa Vermont kwa kutumia fomu inayotolewa na Katibu.

Maudhui ya Malalamishi

Malalamishi ya mchakato faafu lazima yajumuishe:

1. Jina la mtoto;
2. Anwani ya makazi ya mtoto;
3. Jina la shule ambapo mtoto anahudhuria;
4. Ikiwa mtoto au kijana hana makazi, taarifa ya mawasiliano ya mtoto na jina la shule ya mtoto;
5. Maelezo ya hali ya tatizo la mtoto huyo linalohusiana na hatua iliyopendekezwa au iliyokatazwa, ikiwemo taarifa zinazohusiana na tatizo hili; na:
6. Suluhu linalopendekezwa kwa tatizo hilo kwa kiwango ambacho kinajulikana na kupatikana kwako au kwa wilaya ya shule au kwa muungano wa usimamizi kwa wakati huo.

Notisi inahitajika kabla ya kikao cha malalamishi ya mchakato faafu

Wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi huenda msiwe na kikao cha mchakato faafu hadi pale wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi (au wakili wako au wakili wa wilaya ya shule au wa muungano wa usimamizi), atawasilisha malalamishi ya mchakato faafu yanayojumuisha taarifa iliyoorodheshwa hapo juu.

Utoshelevu wa Malalamishi

Ili malalamishi ya mchakato faafu yaende mbele, lazima yazingatiwe kuwa toshelevu. Malalamishi ya mchakato faafu yatazingatiwa kuwa toshelevu (kuwa yamefikisha mahitaji yaliyo hapo juu ya kimaudhui) isipokuwa kama mhusika anayepokea malalamishi hayo ya mchakato faafu (wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi) atamfahamisha afisa mwamuzi na wahusika wengine katika maandishi, ndani ya siku 15 za kalenda baada ya kupokea malalamishi hayo, kwamba mhusika anayepokea anaamini kwamba malalamishi hayo ya mchakato faafu hayatimiza mahitaji yaliyoorodheshwa hapo juu.

Ndani ya siku tano za kalenda tangu kupokea notisi kwamba mhusika anayepokea (wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi) anazingatia malalamishi ya mchakato faafu kuwa na upungufu, afisa mwamuzi lazima aamue iwapo malalamishi hayo ya mchakato faafu yanatimiza mahitaji yaliyoorodheshwa hapo juu, na kukufahamisha wewe na wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi mara moja katika maandishi.

Marekebisho ya Malalamishi

Wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi mnaweza kufanya marekebisho kwenye malalamishi ikiwa tu:

1. Wahusika wengine wataridhia marekebisho hayo katika maandishi na watapewa nafasi ya kutatua malalamishi ya mchakato faafu kupitia mkutano wa kusuluhisha, ulioelezwa hapa chini; au:
2. Katika kipindi kisichozidi siku tano kabla ya kikao cha mchakato faafu kuanza, afisa wa kikao atatoa ruhusa kufanya marekebisho.

Ikiwa mhusika anayelalamika (wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi) atafanya marekebisho kwa malalamishi ya mchakato faafu, ratiba ya mkutano wa kusuluhisha (ndani ya siku 15 za kalenda tangu kupokea malalamishi) na muda uliotengwa kwa usuluhishaji (ndani ya siku 30 za kalenda tangu kupokea malalamishi) utanza tena tarehe ya kuwasilisha marekebisho ya malalamishi.

Majibu ya wilaya ya shule au muungano wa usimamizi kwa malalamishi ya mchakato faafu

Ikiwa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi haujatuma Notisi ya Awali katika Maandishi, kuhusu suala lililomo katika malalamishi yako ya mchakato faafu, wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima, ndani ya siku 10 za kalenda tangu kupokea malalamishi ya mchakato faafu, ukutumie majibu yatakayojumuisha:

1. Maelezo ya kwa nini wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ulipendekeza au kukataa kuchukua hatua iliyoibuliwa katika malalamishi ya mchakato faafu;
2. Maelezo ya chaguzi nyingine ambazo Timu ya mpango wa elimu wa mtu binafsi (IEP) ya mtoto wako ilizingatia na sababu kwa nini chaguzi hizo zilikataliwa;

3. Maelezo ya kita utaratibu wa tathmini, rekodi, au ripoti ambazo wilaya ya shule au muungano wa usimamizi umetumia kama msingi wa hatua iliyopendekezwa au kukataliwa; na:
4. Maelezo ya masuala mengine ambayo ni muhimu kwa hatua iliyopendekezwa au kukataliwa na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi.

Kutoa taarifa kuhusu vipengele 1-4 hapo juu hakuzuii wilaya ya shule au muungano wa usimamizi kushikilia kwamba malalamishi yako ya mchakato faafu yana upungufu.

Majibu ya wahusika wengine kwa malalamishi ya mchakato faafu

Kando na ilivyoelezwa katika mada ndogo iliyo hapa juu, *Majibu ya wilaya ya shule au muungano wa usimamizi kwa malalamishi ya mchakato faafu*, mhusika anayepokea malalamishi ya mchakato faafu lazima, ndani ya siku 10 tangu kupokea malalamishi hayo, awatumie wahusika wengine majibu ambayo yanasughulikia mahususi masuala yaliyomo kwenye malalamishi.

Mifano ya Fomu

Wakala wa Elimu wa Vermont yuko na mfano wa fomu kukusaidia kuwasilisha malalamishi ya mchakato faafu na malalamishi ya kiutawala. Hata hivyo, Jimbo lako au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi huenda usikuhitaji kutumia fomu hizi. Kwa hakika, unaweza kutumia fomu hii au fomu nyingine inayofaa, almradi inajumuisha taarifa inayohitajika katika kuwasilisha malalamishi ya mchakato faafu au malalamishi ya kiutawala.

- Malalamishi ya mchakato faafu: [kwa wazazi](#)
- Malalamishi ya mchakato faafu: [kwa wilaya za shule](#)
- [Fomu ya malalamishi ya kiutawala](#)

34 CFR §300.509

Upatanishi

Kanuni 2365.1.4; 34 CFR §300.506

Jumla

Wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima utoe fursa ya upatanishi kukuruhusu wewe na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi kusuluhisha kutokubaliana kunakohusu suala lolote katika Sehemu B ya IDEA, ikiwemo masuala yanayoibuka kabla ya kuwasilisha malalamishi ya mchakato faafu. Kwa hivyo, upatanishi upo kusuluhisha migogoro ya Sehemu B ya IDEA ikiwa umewasilisha malalamishi ya mchakato faafu au kuomba kikao cha mchakato faafu kama ilivyoelezwa chini ya anwani Kuwasilisha Malalamishi ya Mchakato Faafu.

Mahitaji

Utaratibu huu lazima uhakikishe kuwa mchakato wa upatanishi:

1. Ni wa hiari kwa upande wako na kwa upande wa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi;
2. Hautumiwi kukunyima au kuchelewesha haki yako kwa kikao cha mchakato faafu, au kukunyima haki nyingine yoyote kwa mujibu wa IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont: na:
3. Unaendeshwa na mpatanishi aliyehitimu na asiye na upendeleo ambaye amefunzwa mbinu mwafaka za upatanishi.

Wakala wa Elimu wa Vermont yuko na orodha ya watu ambao ni wapatanishi waliohitimu na wasiokuwa na upendeleo na wanaojua sheria na masharti yanayohusu utoaji wa elimu maalum na huduma zinazohusiana.

Wakala wa Elimu wa Vermont anawajibikia gharama za mchakato wa upatanishi, ikiwemo gharama za mikutano.

Kila mkutano katika mchakato wa upatanishi lazima upangwe kwa wakati ufaao na kuendeshwa katika mahali ambapo ni faafu kwako na kwa wialaya ya shule au muungano wa usimamizi.

Iwapo wewe na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi mtasuluhisha mgogoro kupitia mchakato wa upatanishi, wahusika wote wawili lazima waingie katika mkataba wa kisheria ambao unaeleza suluhisho na:

1. Kueleza kuwa majadiliano yote ambayo yalifanyika katika mchakato wa upatanishi yatabaki siri na hayawezi kutumiwa kama ushahidi katika kikao chochote kitakachofuata cha mchakato faafu au kesi ya madai; na:
2. Yanatiwa sahihi na wewe na mwakilishi wa wilaya ya shule au wa muungano wa usimamizi ambaye ana mamlaka ya kushurutisha wilaya ya shule au muungano wa usimamizi.

Mkataba wa upatanishi katika maandishi na uliotiwa sahihi unatekelezeka katika mahakama yoyote ya Jimbo yenye mamlaka (mahakama ambayo ina mamlaka ya kusikiza kesi kama hii kwa mujibu wa sheria za Jimbo) au katika mahakama ya wilaya ya Marekani.

Majadiliano yanayotokea wakati wa mchakato wa upatanishi lazima yawe siri. Hayawezi kutumiwa kama ushahidi katika kikao chochote kitakachofuata cha mchakato faafu au kesi ya madai katika mahakama yoyote ya Shirikisho au mahakama ya Jimbo au Jimbo linalopokea msaada kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont.

Maombi yaliyoandikwa yatawasilishwa kupitia [Fomu ya Kuomba Utatuzi wa Migogoro kupitia Upatanishi](#), kwa Wakala wa Elimu wa Vermont, Huduma za Upatanishi wa Elimu Maalum, 1 National Life Drive, Davis 5, Montpelier, VT 05620-2501.

Baada ya kupokea ombi kama hilo, wafanyakazi wa Shirikisho watakutumia Notisi ya Haki za Mzazi katika Elimu Maalum na watatuma taratibu zao za upatanishi kwa wahusika wote katika upatanishi huo. Mkataba wa kushiriki upatanishi utakuwa katika maandishi kwenye fomu iliyoidhinishwa na Katibu wa Elimu wa Vermont na kutiwa sahihi na wahusika wote. Ikiwa ombi hilo haliwezi kuwekwa katika maandishi kutokana na sababu za kipekee, kama vile ulemavu wa kuwasiliana katika maandishi, ombi hilo litafanywa kupitia njia nyingine ya mawasiliano.

Mpatanishi kutokuwa na upendeleo

Mpatanishi:

1. Haweza kuwa mwajiriwa wa Wakala wa Elimu wa Vermont au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ambao unahusika katika elimu au utunzaji wa mtoto wako; na:
2. Hapaswi kuwa na masilahi ya kibinafsi au ya kitaalamu ambayo yanakinzana na ukosefu wa upendeleo wa mpatanishi.

Mtu ambaye vinginevyo anastahiki kuwa mpatanishi sio mwajiriwa wa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi au Wakala wa Elimu wa Vermont kwa sababu tu analipwa na Shirika hilo, au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ili kuhudumu kama mpatanishi.

Nafasi ya Mtoto wakati Malalamishi ya Mchakato faafu Yakisubiri Kusikizwa

Isipokuwa kama ilivyoelezwa chini ya anwani *Taratibu Wakati wa Kuwaadibu Watoto mwenye Ulemavu*, pindi malalamishi ya mchakato faafu yametumwa kwa wahusika wengine, katika kipindi cha mchakato wa kusuluhisha, na katika kusubiri uamuzi wa kikao chochote cha mchakato faafu kisichokuwa na upendeleo au kesi mahakamani, isipokuwa pale ambapo wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi mmekubaliana vinginevyo, mtoto wako lazima abaki katika nafasi yake ya sasa ya kielimu.

Ikiwa malalamishi ya mchakato faafu yanahusisha maombi ya kusajiliwa kwanza katika shule ya umma, mtoto wako, kwa kibali chako, lazima asajiliwe katika mpango wa shule ya kawaida ya umma hadi mchakato yote kama hiyo itakapokamilika.

Ikiwa uamuzi wa afisa mwamuzi katika kikao cha mchakato faafu unakubalina na mzazi wa mtoto kwamba kubadilisha nafasi kunafaa, nafasi hiyo itachukuliwa kuwa mkataba baina yako na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi.

Ikiwa malalamishi ya mchakato faafu yanahusisha maombi ya huduma za awali kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont kwa mtoto ambaye anapita kutoka kuhudumiwa kwa mujibu wa Sehemu C ya IDEA hadi Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont na ambaye hastahiki tena huduma za Sehemu C kwa sababu mtoto huyo amefikia umri wa miaka mitatu, wilaya ya shule au muungano wa usimamizi hauhitajiki kutoa huduma za Sehemu C ambazo mtoto huyo amekuwa akipokea. Ikiwa mtoto huyo atapatikana kuwa anastahiki kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont na utaridhia kwa mtoto huyo kupokea elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mara ya kwanza, basi, mkisubiri matokeo ya mchakato huo, wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima utoe elimu hiyo maalum na huduma zinazohusiana ambazo hazina mzozo (ambazo wewe na wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi mnakubaliana).

Kanuni 2365.1.11; 34 CFR §300.518

Mchakato wa Kusuluhisha

Kanuni 2365.1.6.8; 34 CFR §300.510

Mkutano wa Kusuluhisha

Ndani ya siku 15 za kalenda tangu kupokea notisi ya malalamishi yako ya mchakato faafu, na kabla ya kikao cha mchakato faafu kuanza, wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi lazima uandae mkutano nawe na mwanachama au wanachama wanaohusika wa Timu ya mpango wa elimu maalum wa mtu binafsi (IEP) ambao wana ujuzi mahususi wa hoja zilizotambuliwa katika malalamishi yako ya mchakato faafu. Mkutano huo:

1. Lazima ujumuishe mwakilishi wa wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi ambaye ana mamlaka ya kufanya maamuzi kwa niaba ya wilaya ya shule au muungano wa usimamizi; na:
2. Haupaswi kujumuisha wakili wa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi isipokuwa kama wewe umeandamana na wakili wako.

Wewe na wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi mnaamua wanachama wanaohusika wa Timu ya IEP watakaohudhuria mkutano huo.

Lengo la mkutano huo ni kuwawezesha kujadili malalamishi yako ya mchakato faafu, na hoja ambazo zinaweka msingi wa malalamishi hayo, ili wilaya ya shule au muungano wa usimamizi upate fursa ya kutatua mzozo huo.

Mkutano wa kusuluhisha hauhitajiki ikiwa:

1. Wewe na wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi mtakubalina katika maandishi kuachilia mbali mkutano huo; au:
2. Wewe na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi mtakubaliana kutumia mchakato wa upatanishi, kama ilivyoelezwa kwenye anwani *Upatanishi*.

Kipindi cha Upatanishi

Ikiwa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi haujasuluhisha malalamishi ya mchakato faafu kwa kiwango cha kukuridhisha ndani ya siku 30 tangu kupokea malalamishi ya mchakato faafu (katika kipindi cha mchakato wa kusuluhisha), kikao cha mchakato faafu kinaweza kufanyika.

Kipindi cha siku 45 za kalenda cha kutoa uamuzi wa mwisho kinaanza pale siku 30 za kalenda za kipindi cha kusuluhisha zinapoisha, isipokuwa pale ambapo kutafanywa marekebisho fulani kwa kipindi cha kusuluhisha cha siku 30 za kalenda, kama ilivyoelezwa hapa chini.

Isipokuwa pale ambapo wewe na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi mmekubaliana kuachilia mbali mchakato wa kusuluhisha au kutumia upatanishi, ukikosa kushiriki katika mkutano wa kusuluhisha utachelewesha muda wa mchakato wa kusuluhisha na kikao cha mchakato faafu hadi utakapokubali kushiriki katika mkutano.

Iwapo baada ya kufanya juhudi zinazofaa na kurekodi juhudi kama hizo, wilaya ya shule au muungano wa usimamizi hauwezi kupata ushiriki wako katika mkutano wa kusuluhisha, wilaya ya shule au muungano wa usimamizi unaweza, kufikia mwishoni mwa kipindi kusuluhisha cha siku 30 za kalenda, kuomba kwamba afisa mwamuzi atupilie mbali malalamishi yako ya mchakato faafu. Rekodi za juhudi kama hizo zinajumuisha rekodi za majaribio ya wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ya kupanga muda na mahali ambao mnakubalina nyote, kama vile:

1. Rekodi za kina za simu zilizopigwa au majaribio ya kupiga simu na matokeo ya simu hizo; nakala za barua ulizotumiwa na majibu yoyote yaliyopokelewa; na:
2. Rekodi za kina za ziara zilizofanywa nyumbani kwako au mahali pa ajira na matokeo ya ziara hizo.

Ikiwa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi utashindwa kufanya mkutano wa kusuluhisha ndani ya siku 15 za kalenda tangu kupokea notisi ya malalamishi yako ya mchakato faafu au watakosa kushiriki katika mkutano wa kusuluhisha, unaweza kuomba afisa mwamuzi kuamuru kwamba ratiba ya siku 45 za kalenda kwa kikao cha mchakato faafu ianze.

Marekebishi ya kipindi cha kusuluhisha cha siku 30 za kalenda

Ikiwa wewe na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi mtakubaliana katika maandishi kuachilia mbali mkutano wa kusuluhisha, basi ratiba ya siku 45 za kalenda ya kuanza kwa kikao cha mchakato faafu itaanza siku inayofuata.

Baada ya kuanza kwa upatanishi au mkutano wa kusuluhisha na kabla ya kipindi cha siku 30 za kalenda cha kusuluhisha kukamilika, ikiwa wewe na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi mtakubaliana katika maandishi kwamba makubaliano hayaweze kani, basi ratiba ya siku 45 za kalenda ya kuanza kwa kikao cha mchakato faafu itaanza siku inayofuata.

Ikiwa wewe na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi mtakubaliana kutumia mchakato wa upatanishi, kufikia mwisho wa kipindi cha kusuluhisha cha siku 30 za kalenda, wahusika wote wawili wanaweza kukubaliana katika maandishi kuendelea na upatanishi hadi pale watafikia mkataba. Hata hivyo, ikiwa wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi utajiondoa kwenye mchakato wa upatanishi, basi ratiba ya siku 45 za kalenda ya kuanza kwa kikao cha mchakato faafu itaanza siku inayofuata.

Mkataba wa maafikiano katika maandishi

Ikiwa uamuzi wa mzozo utafikiwa katika mkutano wa kusuluhisha, wewe na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima mwandikiane mkataba wa kisheria ambao:

1. Itatiwa sahihi na wewe na mwakilishi wa wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi ambaye ako na mamlaka ya kushurutisha wilaya yako ya shule au muungano wa usimamizi; na:
2. Unatekelezeka katika mahakama yoyote ya Jimbo yenye mamlaka (mahakama ya Jimbo ambayo ina mamlaka ya kusikiza kesi kama hiyo) au katika mahakama ya wilaya ya Marekani.

Kipindi cha kukagua Mkataba

Ikiwa wewe na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi mtainigia katika mkataba kutokana na mkutano wa kusuluhisha, mhusika mojawapo (wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi) anaweza kubatilisha mkataba huo ndani ya siku tatu za kazi tangu wakati wewe na wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi mlipotia mkataba huo sahihi.

Vikao vya Malalamishi ya Mchakato Faafu

Kikao cha Mchakato Faafu Kisichokuwa na Upendeleo

Wakati wowote malalamishi ya mchakato faafu yanawasilishwa, wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi unaohusika katika mzozo lazima mpate fursa ya kuwa na kikao cha mchakato faafu kisichokuwa na upendeleo, kama ilivyoielezwa katika Sehemu za *Malalamishi ya Mchakato Faafu na Mchakato wa Kusuluhisha*. Wakala wa Elimu wa Vermont anawajibikia kuitisha vikao vya mchakato faafu.

34 CFR §300.511

Afisa wa Mwamuzi wa Kikao Kisichokuwa na Upendeleo

Katika kiwango cha chini zaidi, afisa mwamuzi:

1. Lazima asiwe mfanyakazi wa Wakala wa Elimu wa Vermont au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ambao unahusika moja kwa moja katika elimu na utunzaji wa mtoto wako. Hata

hivyo, mtu sio mfanyakazi wa shirika kwa kuwa yeye analipwa na shirika kuhudumu kama afisa mwamuzi;

2. Hapaswi kuwa na maslahi ya kibinafsi au ya kitaalamu ambayo yanakinzana na ukosefu wa upendeleo wa afisa huyo katika kikao;
3. Lazima awe wakili aliyesajiliwa;
4. Lazima awe na ujuzi na uelewa wa masharti ya IDEA, na kanuni za Shirikisho na ya Jimbo kuhusu IDEA, na ufasili wa kisheria wa IDEA na mahakama za Shirikisho na za Jimbo; na:
5. Lazima awe na ujuzi na uwezo wa kuendesha vikao, na kufanya na kuandika maamuzi, kulingana na kanuni zinazofaa za kisheria.

Wakala wa Elimu wa Vermont atahifadhi orodha ya watu ambao wanahudumu kama maafisa waamuzi ikijumuisha maelezo ya kuhitimu kwa kila afisa mwamuzi.

Kanuni 2365.1.7

Mada ya kikao cha mchakato faafu

Mhusika (wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi) atakayeomba kikao cha mchakato faafu hawezi kuibua kwenye kikao cha mchakato faafu masuala ambayo hayakushughulikiwa katika malalamishi ya mchakato faafu isipokuwa kama wahusika wengine wataridhia.

Ratiba ya kuomba kikao

Wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima uombe kikao cha mchakato faafu kisichokuwa na upendeleo ndani ya miaka miwili (2) tangu siku ambapo wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ulijua au ulipaswa kujua kuhusu suala linaloshughulikiwa katika malalamishi hayo. Ikiwa unaomba urejeshaji wa gharama za maamuzi ya kibinafsi ya kumweka mtoto katika elimu maalum, lazima uwasilishe malalamishi yako ya mchakato faafu ndani ya siku tisini (90) tangu uamuzi huo.

Kutozingatia ratiba

Ratiba iliyoelezwa hapo juu haihusiki kwako ikiwa hungeweza kuwasilisha malalamishi ya mchakato faafu kwa sababu:

1. Wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ulipotosha mahususi kwamba ulikuwa umesuluhisha tatizo au suala ambalo linaibuliwa katika malalamishi yako; au:
2. Wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ulikataa kukupatia taarifa ambayo ulihitajika kukupa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont.

Haki za kikao

Kanuni 2365.1.6.15; 34 CFR §300.512

Jumla

Mhusika yeyote katika kikao cha mchakato faafu (ikiwemo kikao kinachohusiana na taratibu za kuadibu) ana haki ya:

1. Kuandamana na kushauriwa na wakili na/au watu walio na ujuzi maalum au mafunzo kuhusu matatizo ya watoto walio na ulemavu;

2. Kuwasilisha ushahidi na kukabili, kuuliza maswali, na kuhitaji uwepo wa mashahidi; Kuzuia uingizaji wa ushahidi wowote katika kikao ambao haukuwa umefichuliwa kwa mhusika huyo angalau siku tano za kazi kabla ya kikao hicho;
3. Kupata katika maandishi, au, kwa chaguo lako, rekodi ya neno kwa neno ya kielektroniki ya kikao hicho; na:
4. Kupata katika maandishi, au, kwa chaguo lako, matokeo ya ukweli na maamuzi kielektroniki.

Ufichuzi wa ziada wa taarifa

Wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima mfichuliane tathmini zote zilizokamilishwa kufikia tarehe hiyo na mapendekezo kulingana na tathmini hizo ambazo wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi unakusudia kutumia katika kikao hicho, angalau siku tano za kazi kabla ya kikao cha mchakato faafu.

Afisa mwamuzi anaweza kuzuia mhusika yeyote ambaye anakosa kutii mahitaji haya kuwasilisha tathmini faafu au mapendekezo katika kikao bila ya kibali cha mhusika wa pili.

Haki za mzazi katika vikao

Wazazi wanaohusika katika vikao wana haki ya:

1. Kuwa na mtoto wao pale;
2. Kuweka kikao wazi kwa umma; na:
3. Kupata rekodi za kikao, matokeo ya hoja na maamuzi yanayotolewa bila gharama kwa wazazi.

Maamuzi ya Kikao

Maamuzi ya Afisa mwamuzi

Maamuzi ya afisa mwamuzi kuhusu iwapo mtoto wako alipokea elimu faafu ya umma bila malipo (FAPE) lazima yajikite kwa hoja thabiti.

Katika masuala yanayodai ukiukaji wa kiutaratibu, afisa mwamuzi anaweza kuamua kwamba mtoto wako hakupokea FAPE iwapo tu upungufu wa kiutaratibu:

1. Umeingilia haki ya mtoto wako ya kupata elimu faafu ya umma bila malipo (FAPE);
2. Umeingilia kwa kiasi kikubwa nafasi yako ya kushiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi kuhusu utoaji wa elimu faafu ya umma bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako; au:
3. Umesababisha kunyimwa manufaa ya kielimu.

Kanuni 2365.1.6.16(c); 34 CFR §300.513

Kifungu cha Masharti ya jumla

Hakuna masharti yaliyoelezwa hapo juu ambayo yanaweza kufasiliwa kumzuia afisa mwamuzi kuamuru wilaya ya shule au muungano wa usimamizi kufuata Kanuni za Jimbo la Vermont 2365.1 hadi 2365.2.15 na 4313.1 hadi 4313.7 na sehemu ya ulinzi wa kiutaratibu za kanuni za Shirikisho kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA (34 CFR §§300.500 hadi 300.536).

Ombi tofauti la kikao cha mchakato faafu

Hakuna chochote katika sehemu ya ulinzi wa kiutaratibu ya kanuni za Shirikisho kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA (34 CFR §§300.500 hadi 300.536) ambacho kinaweza kufasiliwa kukuzuia kuwasilisha malalamishi tofauti ya mchakato faafu kuhusu suala tofauti na malalamishi ya mchakato faafu ambayo yamewasilishwa tayari.

Matokeo na uamuzi kwa jopo la ushauri na umma kwa jumla

Wakala wa elimu wa Vermont au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi, (yeyote anayehusika kwa kikao chako) baada ya kufuta taarifa zozote zinazomtambulisha mtu, lazima:

1. Watume matokeo na uamuzi kwa Baraza la Ushauri wa Elimu Maalum la Vermont; na:
2. Wafanye matokeo na maamuzi hayo yapatikane kwa umma.

Rufaa

Makataa ya Uamuzi; Rufaa; Ukaguzi Usio na Upendeleo

Kanuni 2365.1.8 34; CFR §300.514

Makataa ya Uamuzi wa Kikao

Uamuzi uliofanywa katika kikao cha mchakato faafu (ikiwemo kikao kuhusu taratibu za kuadibu) ni wa mwisho, isipokuwa kama mhusika yeyote anayehusika katika kikao hicho (wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi) anaweza kuanzisha hatua ya madai, kama inavyoelezwa hapa.

Ratiba na Urahisi wa Vikao na Ukaguzi

Wakala wa Elimu wa Vermont lazima ahakikishe kwamba katika muda usiozidi siku 45 za kalenda baada ya kipindi cha siku 30 za kalenda za mikutano ya kusuluhisha *au*, kama ilivyoelezwa chini ya mada ndogo *Marekebisho ya kipindi cha kusuluhisha cha siku 30 za kalenda*, katika siku zisizozidi siku 45 za kalenda baada ya kukamilika kwa kipindi kilichorekebisha, kwamba:

1. Uamuzi wa mwisho umefikiwa katika kikao; na:
2. Nakala ya uamuzi imetumwa kwa kila mhusika.

Afisa mwamuzi anaweza kutoa nyongeza maalum za muda zaidi ya siku 45 za kalenda zilizoolezwa hapo juu kufuatia ombi la mhusika mmojawapo, ikiwa:

1. Maendeleo ya kielimu au ustawi wa mtoto hautahatarishwa na kucheleweshwa huko;
2. Mhusika huyo hakuwa na muda wa kutosha kuandaa na kuwasilisha msimamizi wa mhusika huyo katika kikao kwa mujibu wa masharti ya mchakato faafu; na:
3. Haja ya kucheleweshwa ni kubwa kuliko matokeo yoyote ya kifedha au madhara mengine ambayo yanaweza kumwathiri mhusika iwapo kutatokea kucheleweshwa.

Kila kikao na kila ukaguzi unaohusisha mijadala kwa njia ya mdomo lazima uendeshwe wakati na mahali ambapo panafaa kwako na kwa mtoto wako.

Kanuni 2365.1.6.16 (a) na (b); 34 CFR §300.515

Kesi za Madai, Ikiwemo Kipindi cha Muda ambacho Kesi hizo Zinapaswa Kuwasilishwa

Kanuni 2365.1.9; 34 CFR §300.516

Jumla

Mhusika yeyote (wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi) ambaye hakubaliani na matokeo na maamuzi katika kikao cha mchakato faafu (ikiwemo kikao kinachohusiana na taratibu za kuadibu) ako na haki ya kuleta kesi ya madai kuhusu suala ambalo halishughulikiwi katika kikao cha mchakato faafu. Kesi hiyo inaweza kuletwa katika mahakama ya Jimbo yenye mamlaka (mahakama ya Jimbo ambayo iko na mamlaka ya kusikiza kesi kama hii) au katika mahakama wa wilaya ya Marekani bila kuzingatia kiasi cha mzozo.

Kikomo cha Muda

Mhusika (wewe au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi) ambaye analeta kesi atakuwa na siku 90 za kalenda kutoka siku ya uamuzi wa afisa mwamuzi kuwasilisha kesi ya madai.

Taratibu za ziada

Katika kesi yoyote ya madai, mahakama:

1. Itapokea rekodi za shughuli za kiutawala.
2. Itasikiliza ushahidi wa ziada kufuatia maombi yako au maombi ya wilaya ya shule au muungano wa usimamizi; na:
3. Itakita uamuzi wake kwenye uzito wa ushahidi na kutoa afueni ambazo mahakama itaamua kuwa inafaa.

Mamlaka ya mahakama za wilaya

Mahakama za wilaya za Marekani ziko na mamlaka ya kuamua kuhusu kesi zinazoletwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont bila kuzingatia kiasi cha mzozo.

Kanuni ya Masharti ya jumla

Hakuna chochote katika Sehemu B ya IDEA na Sheria za Elimu Maalum za Vermont ambacho kinazuia au kudhibiti haki, taratibu, na afueni zilizopo kwa mujibu wa Katiba ya Marekani, Sheria ya Wamarekani wenye Ulemavu ya 1990, Sehemu ya V ya Sheria ya Urekebishaji ya 1973 (Kifungu cha 504), au sheria nyingine za Shirikisho zinazolinda haki za watoto walio na ulemavu, isipokuwa kama kabla ya kuwasilisha kesi ya madai kwa mujibu wa sheria hizi na kuomba afueni ambazo pia zinapatikana kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont, taratibu za mchakato faafu zilizoelzwa hapo juu lazima zifuatwe kikamilifu kwa kiwango kinachohitajika ikiwa mhusika atawasilisha kesi kwa mujibu wa IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont. Hii ina maana kwamba huenda ukapata vitulizo vilivyopo kwa mujibu wa sheria zingine ambazo zinaingiliana na zile zilizopo kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA, lakini kwa jumla, kupata afueni kwa mujibu wa sheria hizo nyingine lazima kwanza utumie vitulizo vya kiutawala vilivyopo kwa mujibu wa IDEA (k.v., malalamishi ya

mchakato faafu, mkutano wa kusuluhisha, na kikao cha mchakato faafu kisichokuwa na upendeleo) kabla ya kwenda mahakamani moja kwa moja.

Ada za wakili

Kanuni 2365.1.10; 34 CFR §300.517

Jumla

Katika kesi yoyote au shauri lililowasilishwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont, ikiwa utashinda, mahakama, kwa busara yake, inaweza ikatoa fidia ya ada za wakili zinazofaa kama sehemu ya gharama kwako.

Katika kesi yoyote au shauri lililowasilishwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont, mahakama, kwa busara yake, inaweza ikatoa fidia zinazofaa za ada za wakili kama sehemu ya gharama kwa Wakala wa Elimu wa Vermont au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ikiwa watahinda, zilipwe na wakili wako, ikiwa wakili huyo: (a) aliwasilisha malalamishi au kesi ya mahakamani ambayo mahakama inaamua kuwa ya kipuuzi, isiyo na maana, au isiyokuwa na msingi; au (b) aliendelea kufungua madai baada ya kesi kubainishwa wazi kuwa ni a kipuuzi, haina maana, au haina msingi.

Katika kesi yoyote au shauri lililowasilishwa kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont, mahakama, kwa busara yake, inaweza kutoa fidia zinazofaa za ada za wakili kama sehemu ya gharama kwa Wakala wa Elimu wa Vermont au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ikiwa watahinda, uzilipe mwenyewe au wakili wako, ikiwa utaomba kikao cha mchakato faafu au kesi ya mahakamani itawasilishwa baadaye kwa sababu zisizofaa, kama vile kusumbua, kusababisha ucheleweshaji usiohitajika, au kuongeza gharama za kesi au shauri bila sababu.

Fidia za ada

Mahakama itatoa fidia zinazofaa za ada za wakili ifuatavyo:

1. Ada lazima zijikite kwa viwango vinavyotumwa katika jumuiya ambapo kesi au kikao kilifanyika kwa aina na ubora wa huduma zinazotolewa. Hakuna marupurupu au kizidishi kitakachotumiwa katika kuhesabu fidia ya ada zilizotolewa.
2. Fidha haiwezi kutolewa kwa ada na gharama zinazohusiana haziwezi kurejeshwa katika kesi yoyote au shauri kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont kwa huduma zilizotolewa baada ya kupewa ahadi ya suluhu katika maandishi ikiwa:
 - a. Ahadi hiyo itatolewa ndani ya muda uliotengwa na Kanuni 68 ya Kanuni za Shirikisho kwa Taratibu za Kesi za Madai, au katika hali ya kikao cha mchakato faafu au ukaguzi katika kiwango cha Jimbo, wakati wowote zaidi ya siku 10 za kalenda kabla ya shauri kuanza;
 - b. Ahadi haitakubalika ndani ya siku 10 za kalenda; na:
 - c. Mahakama au afisa mwamuzi wa kikao cha kiutawala atapata kuwa vitulizo ambavyo umepata hatimaye havina nafuu zaidi kuliko ahadi ya suluhu. Licha ya vikwazo hivi, utoaji wa fidia ya ada za wakili na gharama zinazohusiana unaweza kufanywa ikiwa utashinda na iwe kwamba ulikuwa na sababu za kutosha kukataa ahadi ya suluhu.
3. Ada haziwezi kutolewa fidia zinazohusu mkutano wowote wa Timu ya mpango wa elimu wa mtu binafsi (IEP) isipokuwa kama mkutano ulifanyika kutokana na shauri ya kiutawala au kesi ya mahakamani. Ada haziwezi kutolewa fidia kwa upatanishi kama ilivyoielezwa chini ya anwani *Upatanishi*.

Mkutano wa kusuluhisha, kama ulivyoelezwa chini ya anwani Mkutano wa Kusuluhisha, hauzingatiwi kuwa mkutano uliopangwa kutokana na shauri ya kikao au kesi ya mahakamani, na hauzingatiwi kuwa kikao cha kiutawala au kesi ya mahakamani kwa ajili ya masharti haya ya ada za wakili.

Mahakama inapunguza, inavyofaa, kiasi cha ada za wakili zinazotolewa fidia kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont, ikiwa mahakama itabaini kuwa:

1. Wewe, au wakili wako, wakati wa kesi hiyo au shauri, mlichelewesha bila sababu utatuzi wa mwisho wa mgogoro;
2. Kiasi cha ada za wakili ambacho vinginevyo kimetolewa fidia kinazidi kiwango cha kawaida kinachotozwa kwa saa katika jumuiya hiyo kwa huduma sawa na mawakili walio na ujuzi, sifa, na tajriba sawa;
3. Muda ulitoumika na huduma za kisheria zilizowasilishwa zilipita kiasi kwa kuzingatia aina ya kesi au shauri; au:
4. Wakili anayekuwakilisha hakupatia wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi taarifa faafu katika notisi ya kuomba kikao cha mchakato faafu kama ilivyoelezwa chini ya anwani Malalamishi ya Mchakato Faafu.

Hata hivyo, mahakama haiwezi kupunguza ada ikiwa mahakama itabaini kuwa Jimbo au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ulichelewesha utatuzi wa mwisho wa kesi au shauri bila sababu au kulikuwa na ukiukaji wa masharti ya ulinzi wa kiutaratibu ya Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont.

Taratibu Wakati wa Kuadibu Watoto Walio na Ulemavu

Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule

Kanuni 4313.1; 34 CFR §300.530

Uamuzi kwa kila kesi

Wafanyakazi wa shule wanaweza kuzingatia hali zozote za kipekee kwa msingi wa kila kesi, wakati wanaamua iwapo ubadilishaji wa nafasi, unaofanywa kwa mujibu wa mahitaji yafuatayo yanayohusiana na nidhamu, ni faafu kwa mtoto mwenye ulemavu anayekiuka kanuni za shule za mwenendo wa mwnafunzi.

Jumla

Kwa kadri wanavyochukua hatua kama hiyo kwa watoto wasio na ulemavu, wafanyakazi wa shule wanaweza, kwa muda usiozidi siku 10 za shule zikifuatana, kumwondoa mwanafunzi mwenye ulemavu ambaye anakiuka kanuni za shule za mwenendo wa mwanafunzi kutoka kwa nafasi yake ya sasa hadi mazingira mbadala ya kielimu yanayofaa kwa muda (ambayo lazima yaamuliwe na Timu ya mtoto wako ya mpango wa elimu wa mtu binafsi (IEP)), mazingira mengine, au kumwondoa mwanafunzi huyo kwa muda. Wafanyakazi wa shule wanaweza kuweka uondoaji wa ziada kwa mtoto huyo kwa muda usiozidi siku 10 za shule zikifuatana katika mwaka huo wa masomo kwa matukio tofauti ya ukiukaji, almradi uondoaji huo haufasiliwi kuwa ubadilishaji wa nafasi (tazama Ubadilishaji wa Nafasi Kutokana na Uondoaji wa Kinidhamu upate ufasihi, hapa chini).

Baada ya mtoto mwenye ulemavu kuondolewa kutoka kwa nafasi yake ya sasa kwa jumla ya siku 10 za shule katika mwaka sawa wa masomo, wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi lazima, katika siku za uondoaji zitakazofuata katika mwaka huo wa masomo, watoe huduma kwa kiwango kinachohitajika hapa chini ya anwani ndogo Huduma.

Mamlaka ya Ziada

Ikiwa mwenendo uliokiuka kanuni za mwenendo wa mwanafunzi ulikuwa udhihirisho wa ulemavu wa mtoto huyo (tazama Uamuzi wa Udhihirisho, hapa chini) na mabadiliko ya nafasi kwa msingi wa kinidhamu ungezidi siku 10 za shule zikifuatana, wafanyakazi wa shule wanaweza kutumia taratibu za kinidhamu kwa mtoto huyo mwenye ulemavu kwa njia sawa na kwa kiwango sawa kama ingetukia kwa watoto wasiokuwa na ulemavu, isipokuwa kama shule lazima itoe huduma kwa mtoto huyo kama ilivyoelezwa hapa chini ya anwani Huduma. Timu ya IEP ya mtoto huyo itaamua mazingira mbadala ya kielimu ya muda kwa huduma kama hizo.

Huduma

Huduma ambazo lazima zitolewe kwa mtoto mwenye ulemavu ambaye ameondolewa kutoka kwa nafasi yake ya sasa zinaweza kutolewa kwa muda katika mazingira mbadala ya kielimu.

Wilaya ya shule au muungano wa usimamizi unahitajika tu kutoa huduma kwa mtoto mwenye ulemavu ambaye ameondolewa kutoka kwa nafasi yake ya sasa kwa siku 10 za shule au chini katika mwaka huo wa masomo, ikiwa wao hutoa huduma kwa mtoto asiye na ulemavu ambaye ameondolewa kwa njia sawa.

Mtoto mwenye ulemavu ambaye ameondolewa kutoka kwa nafasi yake ya sasa kwa zaidi ya siku 10 za shule lazima:

1. Aendelee kupokea huduma za kielimu, ili kumwezesha mtoto huyo kushiriki katika mtaala wa jumla wa elimu, japo katika mazingira tofauti, na kuendelea katika kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto huyo; na:
2. Apokee, inavyostahili, tathmini ya mwenendo ya utendaji, na huduma za uingiliaji na urekebishaji wa mwenendo, kama ilivyopangwa kushughulikia ukiukaji wa mwenendo ili usitukie tena.

Baada ya mtoto mwenye ulemavu kuondolewa kutoka kwa nafasi yake ya sasa kwa siku 10 za shule katika mwaka sawa wa masomo, na kama uondoaji wa sasa ni wa siku 10 za shule zikifuatana au chini na ikiwa uondoaji sio mabadiliko ya nafasi (tazama ufasihi hapa chini), basi wafanyakazi wa shule, kwa ushauriano na angalau mwalimu mmoja wa mtoto huyo, wataamua kiwango ambacho huduma

zinahitajika kumwezesha mtoto huyo kuendelea kushiriki katika mtaala wa jumla wa elimu, japo katika mazingira tofauti, na kuendelea katika kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto huyo.

Ikiwa uondoaji ni mabadiliko ya nafasi (tazama ufasili hapa chini), Timu ya IEP ya mtoto huyo itaamua huduma faafu kumwezesha mtoto kuendelea kushiriki katika mtaala wa jumla wa elimu, japo katika mazingira tofauti, na kuendelea katika kufikia malengo yaliyowekwa katika IEP ya mtoto huyo.

Uamuzi wa Udhihirisho

Ndani ya siku 10 baada ya uamuzi wowote wa kubadilisha nafasi ya mtoto mwenye ulemavu kwa sababu ya ukiukaji wa mwenendo wa mwanafunzi shuleni (isipokuwa kwa uondoaji wa siku 10 za shule au chini na ambao haubadilishi nafasi), wilaya ya shule au muungano wa usimamizi, mzazi, na wanachama wa Timu ya IEP wanaohusika (kama itakavyobainishwa na mzazi na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi) lazima wakague taarifa yote muhimu kwenye faili ya mwanafunzi, ikiwemo IEP ya mtoto, maoni ya mwalimu, na taarifa yoyote uliyoitoa ili kuamua:

1. Ikiwa mwenendo unaoangaziwa ulisababishwa na, au ulihusiana moja kwa moja au kwa kiasi kikubwa na, ulemavu wa mtoto huyo; au:
2. Ikiwa mwenendo unaoangaziwa ulisababishwa moja kwa moja na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi kushindwa kutekeleza IEP ya mtoto huyo.

Ikiwa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi, mzazi, na wanachama wa Timu ya IEP ya mtoto wataamua kwamba hali mojawapo kati ya hizi imetimizwa, mwenendo lazima uamuliwe kuwa udhihirisho wa ulemavu wa mtoto.

Ikiwa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi, mzazi, na wanachama wa Timu ya IEP ya mtoto wataamua kwamba mwenendo unaoangaziwa ulisababishwa moja kwa moja na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi kushindwa kutekeleza IEP, wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi lazima uchukue hatua mara moja kurekebisha upungufu huo.

Uamuzi kwamba mwenendo ulikuwa udhihirisho wa ulemavu wa mtoto

Ikiwa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi, mzazi na wanachama wa Timu ya IEP wanaohusika wataamua kwamba mwenendo ulikuwa udhihirisho wa ulemavu wa mtoto, Timu ya IEP lazima ama:

1. Iendeshe tathmini ya mwenendo wa utendaji, isipokuwa kama wilaya ya shule au muungano wa usimamizi tayari ulikuwa umeendesha tathmini ya mwenendo ya utendaji kabla ya mwenendo ambao ulisababisha mabadiliko ya nafasi kutokea, na kutekeleza mpango wa uingiliaji wa kimwenendo kwa mtoto huyo; au
2. Ikiwa mpango wa uingiliaji wa kimwenendo tayari ulikuwa umeundwa, ikague mpango huo wa uingiliaji wa kimwenendo, na iurekebishe, kama inavyohitajika, kushughulikia mwenendo husika.

Isipokuwa kama ilivyoelezwa hapa chini kwenye mada ndogo ya hali za kipekee, wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi lazima umrejeshe mtoto huyo kwa nafasi ambayo alikuwa ameondolewa, isipokuwa kama wewe na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi mtakubaliana kubadilisha nafasi yake kama sehemu ya marekebisho ya mpango wa uingiliaji wa kimwenendo.

Hali za Kipekee

Ikiwa tabia hiyo ilikuwa udhihirisho wa ulemavu wa mtoto au la, wafanyakazi wa shule wanaweza kumwondoa mwanafunzi na kumpeleka kwa mazingira mbadala ya kielimu kwa muda (yatakayoamuliwa na Timu ya IEP ya mtoto) kwa hadi siku 45 za shule, ikiwa mtoto huyo:

1. Atabeba silaha (tazama ufasili hapa chini) shuleni au atakuwa na silaha shuleni, kwenye majengo ya shule, au katika shughuli ya shule iliyo chini ya mamlaka ya Wakala wa Elimu wa Vermont au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi;
2. Kwa hiari ametumia au anatumia dawa za kulevya (tazama ufasili hapa chini), au anatumia au atanunua mihadarati, (tazama ufasili hapa chini), akiwa shuleni, kwenye majengo ya shule, au katika shughuli ya shule iliyo chini ya mamlaka ya Wakala wa Elimu wa Vermont au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi; au:
3. Amesababisha marejaha ya mwili (tazama ufasili hapa chini) kwa mtu mwingine akiwa shuleni, kwenye majengo ya shule, au katika shughuli ya shule iliyo chini ya mamlaka ya Wakala wa Elimu wa Vermont au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi.

Ufasili

Mihadarati inamaanisha dawa au muhadarati wowote uliobainishwa kwenye nyongeza I, II, III, IV, au V katika kipengele cha 202(c) cha Sheria ya Mihadarati (21 U.S.C. 812(c)).

Dawa za Kulevya inamaanisha muhadarati ambao umedhibitiwa; lakini hajumuishi muhadarati ambao unamilikiwa kihalali au unaotumiwa chini ya uangalizi wa mtaalamu wa afya aliye na leseni au unaomilikiwa au kutumiwa kwa mujibu wa mamlaka ya Sheria hiyo na masharti mengine ya Sheria ya Shirikisho.

Majeraha mabaya ya mwili ina maana ya maana inayotolewa kwa dhana “majeraha mabaya ya mwili” katika ibara ya (3) ya kifungu cha (h) cha kipengele 1365 cha sehemu ya 18, Kanuni za Marekani.

Silaha ina maana iliyotolewa kwa “silaha hatari” katika aya ya (2) ya kifungu cha (g) cha kipengele cha 930 sehemu ya 18 ya Kanuni za Marekani.

Taarifa

Mnamo siku ya kufanya uamuzi wa uondoaji ambao ni kubadilisha nafasi mtoto kwa sababu ya ukiukaji wa kanuni za mwenendo wa mwanafunzi, wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima umfahamishe mzazi kupitia notisi ya ulinzi wa kiutaratibu.

Kubadilisha Nafasi Kwa Sababu ya Uondoaji wa Kinidhamu

Uondoaji wa mtoto mwenye ulemavu kutoka kwa nafasi yake ya kielimu ya sasa ni kubadilisha nafasi ikiwa:

1. Uondoaji ni wa zaidi ya siku 10 za shule zikifuatana; au:
2. Mtoto huyo amehusika katika msururu wa uondoaji ambao unaashiria ruwaza kwa sababu:
 - a. Msururu huo wa uondoaji una jumla ya zaidi ya siku 10 za shule katika mwaka wa masomo;
 - b. Mwenendo wa mtoto unafanana kwa kiasi kikubwa na mwenendo wake katika matukio ya hapo awali ambayo yaliishia kwa msururu wa uondoaji;
 - c. Masuala ya ziada kama vile urefu wa kila uondoaji, jumla ya muda ambao mtoto ameondolewa, na muda baina ya uondoaji mmoja na mwingine; na:
 - d. Ikiwa ruwaza ya uondoaji inachangia mabadiliko ya nafasi yataamuliwa kwa msingi wa kila tukio na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi na, ikiwa kutakuwa na pingamizi, inaweza kukaguliwa kupitia shauri za mchakato faafu na za kesi mahakamani.

Kanuni 4313.7 34; CFR §300.536

Uamuzi wa Mazingira

Timu ya mpango wa elimu wa mtu binafsi (IEP) lazima iamue mazingira mbadala ya kielimu ya muda kwa uondoaji ambao ni ubadilishaji wa nafasi, na uondoaji kwa mujibu wa anwani *Mamlaka ya Ziada na Hali za Kipekee*, hapo juu.

Kanuni 4313.2 34; CFR § 300.531

Rufaa

Kanuni 4313.3; 34 CFR § 300.532

Jumla

Mzazi wa mtoto mwenye ulemavu anaweza kuwasilisha malalamishi ya mchakato faafu (tazama hapo juu) kuomba kikao cha mchakato faafu ikiwa hajakubaliana na:

1. Uamuzi wowote kuhusu nafasi uliofanywa kwa mujibu wa masharti haya ya nidhamu; au:
2. Uamuzi wa Udhahirisho ulioelezwa hapo juu.

Wilaya ya shule au muungano wa usimamizi unaweza kuwasilisha malalamishi ya mchakato faafu (tazama hapo juu) kuomba kikao cha mchakato faafu ikiwa wanaamini kwamba kudumisha nafasi ya sasa ya mtoto kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha jeraha kwa mtoto huyo au kwa wengine.

Mamlaka ya afisa mwamuzi

Afisa mwamuzi wa kikao ambaye anatimiza mahitaji yaliyoelezwa chini ya mada ndogo *Afisa Mwamuzi wa Kikao Kisichokuwa na Upendeleo* lazima aendeshe kikao cha mchakato faafu na kufanya uamuzi. Afisa mwamuzi anaweza:

1. Kumrejisha mtoto mwenye ulemavu katika nafasi ambayo alikuwa ametolewa, ikiwa afisa mwamuzi ataamua kwamba uondoaji ulikuwa ukiukaji wa mahitaji yaliyoelezwa chini ya mada Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule, au kwamba mwenendo wa mtoto ulikuwa udhihirisho wa ulemavu wa mtoto huyo; au:
2. Akaamuru kubadilishwa kwa nafasi ya mtoto mwenye ulemavu hadi mazingira mbadala ya muda ya kielimu ambayo yanafaa kwa muda usiozidi siku 45 za shule ikiwa afisa mwamuzi ataamua kwamba kudumisha nafasi ya sasa ya mtoto kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha jeraha kwa mtoto huyo au kwa wengine.

Taratibu hizi za kikao zinaweza kurudiwa, ikiwa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi unaamini kwamba kumrejisha mtoto kwa nafasi ya awali kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha jeraha kwa mtoto huyo au kwa wengine.

Wakati wowote mzazi au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi utawasilisha malalamishi ya mchakato faafu kuomba kikao cha haraka, kikao kinachotimiza mahitaji yaliyoelezwa chini ya mada *Taratibu za Malalamishi ya Mchakato Faafu, Vikao vya Malalamishi ya Mchakato Faafu* lazima kifanyike, isipokuwa ifuatavyo:

1. Ikiwa mzazi hakubaliani na nafasi ya muda au mbadala, au LEA anaamini kwamba nafasi ya sasa ina uwezekano mkubwa wa kusababisha jeraha kwa mtoto huyo au mtu mwingine, Wakala wa Elimu wa Vermont lazima apange kikao cha haraka cha mchakato faafu, ambacho lazima kifanyike ndani ya siku 20 za shule tangu siku ya maombi ya kikao na lazima wafikie uamuzi ndani ya siku 10 za shule baada ya kikao.
2. Isipokuwa kama wazazi na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi utakubali katika maandishi kuacha kudai mkutano huo, au watakubali kutumia upatanishi, mkutano wa kusuluhisha lazima ufanyike ndani ya siku saba za kalenda tangu kupokea notisi ya malalamishi ya mchakato faafu. Kikao kinaweza kuendelea isipokuwa kama suala limetatuliwa kwa njia ya kuridhisha pande zote mbili ndani ya siku 15 za kalenda tangu kupokea malalamishi ya mchakato faafu.

Mhusika anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa kikao cha haraka cha mchakato faafu sawa na anavyoweza kufanya kwa maamuzi katika vikao vingine vya mchakato faafu (tazama *Rufaa*, hapo juu).

Nafasi Wakati wa Rufaa

Wakati, kama ilivyoelezwa hapo juu, mzazi au wilaya ya shule au muungano wa usimamizi umewasilisha malalamishi ya mchakato faafu yanayohusiana na masuala ya kinidhamu, mtoto lazima (isipokuwa kama mzazi na wilaya ya shule au muungano wa usimamizi watakubaliana vinginevyo) abaki katika mazingira mbadala ya muda ya kielimu akisubiri uamuzi wa afisa mwamuzi, au hadi kumalizika kwa muda wa kuondolewa kama ulivyoelezwa chini ya mada Mamlaka ya Wafanyakazi wa Shule, chochote kitakachotokea kwanza.

Kanuni 4313.4; 34 CFR §300.533

Ulinzi Kwa Watoto Ambao Bado Hawastahiki Elimu Maalum na Huduma Zinazohusiana

Kanuni 4313.5; 34 CFR §300.534

Jumla

Ikiwa mtoto hajabainishwa kuwa anastahiki elimu maalum na huduma zinazohusiana na akakiuka kanuni za mwenendo wa mwanafunzi, lakini wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ulikuwa na ufahamu, (kama ilivyoelezwa hapa chini) kabla ya mwenendo ambao ulisababisha hatua za kuadibu kutokea, kuwa mtoto huyo alikuwa mtoto mwenye ulemavu, basi mtoto huyo anaweza kudai ulinzi wowote ulioelezwa katika notisi hii.

Msingi wa ufahamu kwa masuala ya kinidhamu

Wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima uchukuliwe kuwa na ufahamu kwamba mtoto fulani ni mtoto mwenye ulemavu ikiwa, kabla ya mwenendo ambao ulisababisha hatua za kuadibu kutokea:

1. Mzazi alikuwa ameeleza shauku katika maandishi kwamba mtoto huyo anahitaji elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa wafanyakazi wa usimamizi au wa kiutawala wa wakala faafu wa kielimu, au kwa mwalimu wa mtoto huyo;
2. Mzazi aliomba tathmini inayohusu ustahiki kwa elimu maalum na huduma zinazohusiana kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont; au:
3. Mwalimu wa mtoto, au mfanyakazi mwingine wa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi alieleza shauku mahususi kuhusu ruwaza ya mwenendo iliyodhihirishwa na mtoto moja kwa moja kwa wilaya ya shule yako au kwa mkurugenzi wa elimu maalum katika muungano wa usimamizi au mfanyakazi mwingine wa usimamizi katika wilaya ya shule au muungano wa usimamizi.

Hali za pekee

Wilaya ya shule au muungano wa usimamizi haungechukuliwa kuwa na ufahamu kama huu ikiwa:

1. Mzazi wa mtoto huyo hajaruhusu tathmini kwa mtoto au amekataza huduma za elimu maalum; au:
2. Mtoto huyo amefanyiwa tathmini na ikabainishwa kuwa si mtoto mwenye ulemavu kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont.

Masharti ambayo yanatumika ikiwa hakuna msingi wa ufahamu

Ikiwa kabla ya hatua za kuadibu dhidi ya mtoto, wilaya ya shule au muungano wa usimamizi hauna ufahamu kwamba mtoto fulani ni mtoto mwenye ulemavu, kama ilivyoelezwa chini ya mada ndogo Msingi wa ufahamu kwa masuala ya kinidhamu na Hali za Kipekee mtoto huyo anaweza kuchukuliwa hatua za kuadibu ambayo inatumika kwa watoto wasiokuwa na ulemavu ambao wamehusika katika mienendo sawa.

Hata hivyo, ikiwa ombi litatolewa kufanya tathmini ya mtoto katika kipindi ambapo mtoto huyo anachukuliwa hatua za kuadibu, tathmini hiyo lazima iendeshe kwa njia ya haraka.

Hadi pale tathmini itakapokamilika, mtoto atabaki katika nafasi ya kielimu iliyoamuliwa na mamlaka za shule, ambayo inaweza kujumuisha uondoaji wa muda au kufukuzwa kabisa bila huduma za kielimu.

Ikiwa mtoto huyo atabainishwa kuwa mtoto mwenye ulemavu, kwa kuzingatia taarifa kutokana na tathmini iliyoendesha na wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi, na taarifa iliyotolewa na mzazi, wilaya ya shule au muungano wa usimamizi lazima utoe elimu maalum na huduma

zinazohusiana kwa mujibu wa Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont, ikiwemo mahitaji ya kuadibu yaliyoelezwa hapo juu.

Rufaa Kwa na Hatua Za Maafisa wa Sheria na Mamlaka za Mahakama

Sehemu B ya IDEA:

1. Haizuii wakala yeyote kuripoti uhalifu unaotekelezwa na mtoto mwenye ulemavu kwa mamlaka zinazofaa; au:
2. Haizuii maafisa wa sheria wa Jimbo na mamlaka za mahakama kutekeleza majukumu yao kuhusu matumizi ya sheria ya Shirikisho na ya Jimbo kwa uhalifu uliotekelezwa na mtoto mwenye ulemavu.

Kanuni 4313.6; 34 CFR §300.535

Utumaji wa rekodi

Ikiwa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi utaripoti uhalifu uliotekelezwa na mtoto mwenye ulemavu, wilaya ya shule au muungano wa usimamizi:

1. Lazima uhakikishe kwamba nakala za elimu maalum na rekodi za kinidhamu za mtoto huyo zinatumwa ili kuzingatiwa na mamlaka ambayo wakala ameripoti uhalifu huo; na:
2. Unaweza kutuma nakala za elimu maalum na rekodi za nidhamu za za mtoto huyo kwa kiwango tu kinachoruhusiwa na Sheria ya Haki za Kielimu kwa Familia na Faragha (FERPA).

Mahitaji ya Uamuzi wa Kibinafsi wa Wazazi wa Watoto Kuwasajili Katika Shule ya kibinafsi kwa Gharama ya Umma

Jumla

Sehemu B ya IDEA na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont hazihitaji wilaya ya shule au muungano wa usimamizi kulipia gharama za elimu, ikiwemo elimu maalum na huduma zinazohusiana, za mtoto wako mwenye ulemavu katika shule ya kibinafsi ikiwa wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ulitoa elimu faafu ya umma ya bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako na ukaamua kumpeleka mtoto huyo katika shule ya kibinafsi. Hata hivyo, wilaya ya shule au muungano wa usimamizi ambapo shule hiyo ya kibinafsi inapatikana lazima ijumuishe mtoto wako katika idadi ya wale ambao mahitaji yao yanashughulikiwa kwa mujibu wa masharti ya Sehemu B na Kanuni za Elimu Maalum za Vermont kuhusu watoto ambao wamesajiliwa na wazazi wao katika shule ya kibinafsi kwa mujibu wa 34 CFR §§300.131 hadi 300.144.

Kanuni 2368.1.4; 34 CFR §300.148

Urejeshaji kwa usajili katika shule ya kibinafsi

Ikiwa mtoto wako hapo awali alipokea elimu maalum na huduma zinazohusiana chini ya mamlaka ya wilaya ya shule au muungano wa usimamizi, na ukachagua kumsajili mtoto wako katika shule ya msingi au ya upili ya kibinafsi bila kibali cha au rufaa ya wilaya ya shule au muungano wa usimamizi, mahakama au afisa mwamuzi anaweza kuelekeza wakala kukurejeshea gharama zako za usajili huo ikiwa mahakama au afisa mwamuzi ataamua kuwa wakala hakuwa ametoa elimu faafu ya umma ya bila malipo (FAPE) kwa mtoto wako kwa njia inayofaa kabla ya usajili huo, na kwamba usajili katika shule ya kibinafsi ulifaa. Afisa mwamuzi au mahakama inaweza kuamua kuwa usajili wako ni faafu, hata kama usajili huo hautimizwi viwango vya Jimbo ambavyo vinahusika kwa elimu inayotolewa na wilaya ya elimu au muungano wa usimamizi.

Ukomo wa Urejeshaji

Ghamara za urejeshaji zilizoelzwa katika aya iliyoko hapa juu zinaweza kupunguzwa au kukatazwa ikiwa:

1. (a) Katika mkutano wa hivi karibuni zaidi wa mpango wa huduma binafsi za elimu (IEP) ambao ulihudhuria kabla ya mtoto wako kuondolewa katika shule ya umma, hukuifahamisha Timu ya IEP kwamba ulikuwa unakataa nafasi iliyokuwa imependekwa na wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi ya kutoa FAPE kwa mtoto wako, na hukueleza shauku zako na nia yako ya kumsajili mtoto wako katika shule ya kibinafsi kwa gharama ya umma; au (b) Angalau siku 10 za kazi (ikiwemo sikukuu zozote ambazo zitatokea katika siku ya kazi) kabla ya kumuondoa mtoto wako kwenye shule ya umma, hukutoa noti ya taarifa hiyo katika maandishi kwa wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi;
2. Ikiwa, kabla ya kumuondoa mtoto wako kutoka shule ya umma, wilaya ya shule yako au muungano wa usimamizi ulikutumia noti ya awali katika maandishi, ya nia yake ya kumfanyia mtoto wako tathmini (ikiwa ni pamoja na taarifa ya azma ya tathmini hiyo ambayo ni faafu na yenye busara), lakini hukuhakikisha mtoto wako anapatikana kwa ajili ya tathmini hiyo; au
3. Mahakama iliamua kwamba hatua zako hazikuwa za busara.

Hata hivyo, gharama za urejeshaji:

1. Lazima zisipunguzwe au kukatazwa kwa kukosa kutoa noti ikiwa: (a) Shule ilikuzuia kutoa noti hiyo; (b) Haukuwa umepokea noti ya wajibu wako wa kutoa noti iliyoelezwa hapo juu (kupokea ulinzi huu wa kiutaratibu); au (c) Uzingatiaji wa mahitaji yaliyo hapo juu huenda ungesababisha madhara ya kimwili kwa mtoto wako; na:
2. Mahakama au afisa mwamuzi, anaweza kutumia busara yake kutopunguza au kukataza urejeshaji kwa sababu ya kukosa kutoa noti inayohitajika ikiwa: (a) Mzazi hajui kusoma na kuandika au hawezi kuandika kwa Kiingereza; (b) Uzingatiaji wa mahitaji yiyoko hapo juu huenda ungesababisha madhara mabaya ya kihisia kwa mtoto wako.